Jumamosi Januari 4, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581912
www.ippmedia.com 0677 020 710
MWANGA WA JAMII
Nipashe digital
LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ
epaper.ippmedia.com



UKURASA 21
**RODRI ATEMA CHECHE KUHUSU BALLON D'OR**

UKURASA 3
**Askofu:** Walimu wasitelekezewe mzigo wa malezi

UKURASA 7
**Mbaroni** tuhuma wizi wa kimtandao

UKURASA 18
**'Special hire'** sasa kuunganishwa VTS



# W'biashara watoa kilio upatikanaji wa Dola

UKURASA 2





Kichwa cha treni ya mchongoko kikisafirishwa kwenye lori maalum kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Stesheni ya Magufuli, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 5

## 'WAPAMBE CHANZO MNYUKANO LISSU, MBOWE'



MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Victoria na mgombea wa Makamu Mwenyekiti Taifa, Ezekia Wenje, amesema wapambe wa Mwenyekiti ...

## Mwinyi: Bil. 300/- kutengwa kila mwezi kulipa deni la nchi

UK. 3

## Kamati za Bunge kujifungia siku 18 Dodoma

UKURASA 5

MICHEZO **YANGA KAZI MOJA USHINDI** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Wapinzani waendelea kutimkia CCM

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANACHAMA 24 wakiwamo viongozi wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wamehamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai kuwa serikali imetekeleza malalamiko yao.

Makada hao ambao kati yao 18 wanatokea CHADEMA, moja ni NCCR-Mageuzi na watano ni kutoka TLP, walifikia uamuzi huo juzi baada ya mkutano wa hadhara wa Mbunge wa jimbo hilo uliolenga kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Mmoja wa makada hao ambaye ni Katibu wa Baraza la Wazee CHADEMA, Jimbo la Ushetu, Emmanuel Machibya, alisema hatua ya serikali kupelekea maendeleo wananchi hasa kwenye sekta ya afya, elimu na maji imewafanya kukosa cha kusema wala kukosoa.

Alisema hiyo ndio sababu kubwa iliyofanya kuachana na vyama vyao na kujiunga na CCM ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Alisema, miongoni mwa vitu walivyokuwa wakivisemea sana na vimetekelezwa ni pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Ushetu na utekelezaji wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria, ambao unakaribia kuwafikia.

"Tunatumia maji ya kwenye visima tulivyochimba wenyewe na vile vilivyochimbwa na RUWASA, na maji ya Ziwa Victoria, tulikuwa tunayatumia pale tunapofika Halmashauri za Msalala na Manispaa ya Kahama na sasa yanakuja kwetu hivyo hatuna haja ya kuendelea kupiga kelele huku miradi inatekelezwa na serikali," alisema Machibya.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), Kata ya Kisuke, Kulwa Chanila alisema, katika mradi wa maji ya Ziwa Victoria, vijana wamepewa ajira zisizohitaji ujuzi za uchimbaji wa mitaro ya bomba, kusogeza bomba nyinginezo na wanajipatia fedha za kuendesha maisha yao na hakuna ubaguzi uliofanywa wa kuwatenga vyama vya upinzani.

Alisema, kitu kingine kilichomvutia ni uwapo wa huduma bora katika vituo vya afya wakati wa kujifungua kulinganisha na awali.

Akipokea wanachama hao wapya, Mbunge Cherehani aliwaahidi kuwapatia ushirikiano na kuendelea kuwahudumiwa wananchi pasi kuwa na ubaguzi wa aina yoyote.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kisuke, Doto Misungwi, alisema ujio wa wanachama hao ndani ya chama chake ni ishara tosha kwamba Ilani ya uchaguzi inatekelezwa kwa vitendo na kuwataka wengine kujitokeza na kujiunga kwa kuwa kile walichokuwa wanakipigia kelele ndio serikali inakitekeleza sasa.



Daraja lililopo eneo la Lilombe wilayani Liwale mkoani Lindi, linalounganisha Wilaya za Nachingwea na Tunduru mkoani Ruvuma likiwa halijawekewa kifusi pembeni kwa miaka miwili kitendo kinachosababisha lisitumike. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara watoa kilio upatikanaji Dola

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wanaonunua bidhaa nje ya nchi wamesema licha ya Dola ya Kimarekani kushuka thamani dhidi ya Shilingi ya kitanzania, upatikanaji wake umeendelea kuwa wa shida na kuwasababishia usumbufu wa kuitafuta hali inayowafanya kuingia hasara kibiashara.

Mapema mwaka 2023, nchi ilikumbwa na uhaba wa Dola nchini uliotokana na kuadimika kwa fedha hiyo katika Soko la Dunia, sababu kuu ikielezwa kuwa ni athari za ugonjwa wa UVIKO 19 uliokumba ulimwengu tangu mwaka 2019 na vita vya Ukraine na Urusi.

Kuadimika kwa fedha hiyo kulisababisha usumbufu kwa wafanyabiashara nchini hasa wanaoagiza bidhaa nje ya nchi kwa kuwa walilazimika kuinunua kwa gharama kubwa hadi Sh. 2,800 kutoka kwa watu binafsi baada ya kukosekana benki.

Hata hivyo, serikali ilifanya juhudi kuimarisha sarafu ikiwamo kuunda kikosi kazi cha wataalamu kilichotafiti hali hiyo na kushauri hatua za kuchukuliwa na kadri siku zilivyosogea dola ilikuwa ikishuka thamani dhidi ya shilingi ya kitanzania.

Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania, juzi fedha hiyo iliuzwa kwa Sh. 2,406 kutoka Sh. 2,700 bei ya Oktoba, mwaka jana, hali iliyokuwa ikisababisha hasara kwa wafanyabiashara nchini.

Mfanyabiashara wa nguo za kike Kariakoo, Ramadhani Ngang'uli alisema walitegemea baada ya dola kushuka thamani ingepatikana kwa urahisi kama ilivyokuwa mwanzo, lakini mambo yamekuwa tofauti.

Alisema wanapokwenda kununua fedha hiyo kwenye benki, wanaikosa na kuendelea na utaratibu wao wa kuitafuta kutoka kwa watu binafsi ambao huwauzia kwa bei ya juu ukilinganishwa na wanayonunulia benki.

Alisema wanalazimika kuitafuta fedha hiyo ili kupunguza gharama za kuagiza mzigo kutokana na baadhi ya mawakala wa usafirishaji kutumia fursa hiyo kuwauzia fedha hiyo kwa bei ya juu.

"Yaani ni kwamba mawakala wa usafirishaji wa mizigo wameshajiwekea utaratibu wao wa kulipia kwa dola kwa hiyo kama huna dola wao ndio wanakupangia 'exchange rate' (gharama za kubadilisha fedha) ambayo ni kubwa kuliko benki au mitaani," alisema.

Mfanyabiashara Lemsi Mazengo, alisema japokuwa upatikanaji wa dola umeimarika kwenye benki, lakini hautimizi haja za wafanyabiashara, akitoa mfano kuwa kwa sasa wanaweza kuuza hadi dola 500 tofauti na hapo awali walikuwa wanauza dola 100 pekee kwa kila mteja tena kwa masharti.

Alitaja moja ya masharti hayo kuwa ili uuziwe fedha hiyo katika benki ni lazima uwe mteja wao wa kila siku uliyefungua akaunti hali iliyokuwa inaleta usumbufu na baadhi kuuziwa 100 pekee kwa siku.

Alisema hata hivyo, bado fedha hiyo imekuwa ikipanda na kushuka akitoa mfano kuwa juzi ilikuwa ikiuzwa Sh. 2,406, lakini jana iliuzwa kwa Sh. 2,500 hali inayoashiria kuwa bado tatizo hilo halijakaa sawa. Alisema hali hiyo pamoja na kuleta usumbufu wa kuitafuta pia wakati mwingine inasababisha hasara, kwa kuwa wanaweza kununua mzigo wakati dola ipo juu, lakini mzigo unaofika na kuanza kuuza, dola inakuwa imeshuka na kulazimika kuuza bei ya chini.

"Unaweza ukanunua mzigo kwa dola ikiwa juu, lakini ikishuka itakulazimu uuze kwa bei ndogo kutokana na kushuka kwake kwa hiyo wakati mwingine unaweza kupata hasara kabisa," alisema Mazengo.

Mfanyabiashara Jabiri Mtoro, alisema, anatambua kama dola imeshuka, lakini yeye anaipata kirahisi kwa sababu ananunua kwa watu binafsi badala ya kwenda benki.

Mfanyakazi wa Benki ya Akiba Commercial (jina tunalihifadhi), alisema upatikanaji fedha kwa sasa umeimarika kuliko zamani na kufikia hatua ya kuuza hadi dola 5000 kwa siku tofauti na miezi sita iliyopita walikuwa wakitoa dola 1000 pekee.

Alisema kinacho sababisha dola kuadimika ni baadhi ya wafanyabishara wakubwa hasa katika sekta ya utalii ambao ndio wanaopokea dola kwa wingi kutozipeleka benki na kuziuza wenyewe mitaani.

Alisema hali hiyo inasababisha benki kukosa fedha za kuuzia wateja kwa sababu wanategemea kupata kutoka kwenye makundi hayo na si Benki Kuu kama wengi wanavyofikiri.

"Hii imekuwa biashara kwa sasa ikishuka wenye mitaji mikubwa wananunua, wanahifadhi wanategemea ikipanda na wao wanauza kwa hiyo tabia hiyo inafanya mzunguko wa dola kuwa mdogo hata kama imeshuka," alisema.

Kadhalika, hali hiyo imekuwa tishio pia kwa wafanyabiashara na wengine wanaogopa kununua bidhaa za gharama kubwa kutokana na kupanda na kushuka kwa fedha hiyo.

**BoT YAFAFANUA**

Ofisa Habari Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Victoria Msina, amesema benki hiyo ilitoa miongozo kwa miamala ya kifedha nchini ifanywe kwa shilingi ya kitanzania na si dola ili kuwaondolea usumbufu na hasara wafanyabiashara.

Amesema hata taarifa mbalimbali wanazozitoa kwa umma kupitia tovuti yao wanahamasisha kutumia Shilingi za Tanzania na kwa sasa inaonekana imepanda thamani ikilinganishwa na Dola ya Marekani.

"Ndio maana serikali inasisitiza wananchi wafanye miamala mbalimbali kutumia fedha zetu hata shule za 'international' wanashauriwa walipe ada kwa kutumia fedha za Tanzania.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# 130 waliokimbia ukeketaji wagoma kurejea nyumbani

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

WASICHANA 130 waliokimbia familia zao kuepukana na kukeketwa wamegoma kurejea nyumbani wakiogopa kutendewa unyanyasaji na wazazi, ndugu au walezi wao.

Wasichana hao ni waliohifadhiwa katika kituo cha ATFGM Massanga wilayani Tarime, mkoani Mara kwa lengo la kulindwa dhidi ya vitendo vya ukeketaji walivyolazimishwa kufanyiwa na wazazi wao.

Meneja miradi wa kituo hicho, Valerian Mgani alisema juzi wakati akipokea misaada iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya watoto hao, kuwa wasichana hao wameogopa kurudi nyumbani wakihofia wazazi wao kuwalazimisha kukeketwa na kuingia katika ndoa za mapema kinyume na matarajio yao.

"Wasichana hao walikimbilia hapa baada ya kulazimishwa kukeketwa na baadhi ya walezi na wazazi wao wasio waaminifu na baada ya muhula wa tohara kukamilika wamegoma kurudi kwao wakihofia kufanyiwa ukatili wa kijinsia," alisema.

Akikabidhi zawadi hizo kwa niaba ya Rais, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele, aliagiza Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Tarime kushiriki mpango wa kuwahudumia wasichana hao wakati serikali ikichukua hatua zaidi kuwanusuru.

Alisema serikali itachukua hatua kwa wazazi wote ambao watakiuka wajibu wao wa kuhudumia familia zao kwa kuzuia watoto hasa wa kike kupata elimu kwa ajili ya kuolewa kwa tamaa ya mali.

Aidha, alisema lazima jamii katika eneo hilo iachane na mila zinazoshusha hadhi ya wanawake na wasichana wadogo.

Kadhalika, aliliagiza Jeshi la Polisi kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria kwa watu wote wanaoendeleza ukeketaji nyakati za usiku na kuwavisha wasichana mavazi ya wanaume ili kukwepa mkono wa sheria.

Alitahadharisha baada ya shule kufunguliwa mwanzoni mwa mwaka huu, kuwa serikali kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji wataanzisha msako kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanajiunga kidato cha kwanza.

# Mwinyi: Bil. 300/- kutengwa kila mwezi kulipa deni la nchi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa serikali inatenga Sh. bilioni 300 kwa mwezi kulipa madeni ya nchi.

Aliyasema hayo jana alipofungua kituo cha mabasi kilichojengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), eneo la Kijangwani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema wakati serikali inakopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ina akaunti maalum inayoweka fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa madeni hayo ambayo sasa inahifadhi ya Sh. bilioni 600.

Alisema deni hilo kwa upande wa Zanzibar kwa sasa ni Sh. trilioni 1.2 linalohimilika kwa kuwa serikali ina uwezo wa kulilipa ndani ya miaka miwili na kukopesheka tena kutokana na utaratibu uliopo.

Alisema wakati wa Serikali ya Awamu ya Nane deni hilo lilikuwa Sh. bilioni 800 ndani ya miaka minne limepanda na kufikia Sh. trilioni 1.2.

Aidha, aliwataka Wazanzibar kupuuzia taarifa zilizotolewa na vyama vya upinzani hivi karibuni kuwa deni hilo limefika Sh. trilioni 2.8 sawa na ongezeko la asilimia 208 akisema ni za upotoshaji na propaganda za kisiasa.

Alisisitiza kuwa serikali inakopa kwa nia njema ya kuendesha miradi ya maendeleo yenye tija na maslahi kwa nchi na sio vinginevyo.

Dk. Mwinyi pia alikemea urasimu unaofanywa na watu wasio waaminifu ndani ya serikali kwa taasisi binafsi zinazotaka kuwekeza nchini na kuzielekeza taasisi hizo kutoa taarifa kwake pale wanapokumbana na changamoto hiyo.

Akizungumzia kituo kipya cha mabasi, Dk. Mwinyi aliagiza ZSSF kuwa na mpango maalum wa matunzo na usafi na kuandaa ajira maalum kwa vijana kwa ajili kutoa huduma za usafi.

**Alisisitiza kuwa serikali inakopa kwa nia njema ya kuendesha miradi ya maendeleo yenye tija na maslahi kwa nchi na sio vinginevyo.**

Alisema serikali inatengeneza mpango mkuu wa usafiri utakaobadilisha mfumo wa sasa kuwa wa kisasa na kutoa huduma bora.

Alisema mpango huo utajumuisha ujenzi wa vituo vya kisasa vya mabasi katika maeneo ya Chuini, Jumbi Mwera, Mwanakwerekwe na Kijangwani, Malindi na Mnazi Mmoja kwa eneo la mjini.

Aidha, alisema kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu Zanzibar itaanza kutumia mabasi ya kutumia umeme.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya Salum, alisema uwekezaji unaofanywa katika miradi mbalimbali nchini unaongeza thamani ya kiuchumi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akili, alisema uchumi wa Zanzibar unategemea sekta za huduma hususan utalii na usafiri kwa asilimia 50.

Alisema pia mifumo ya kisasa ya usafiri inalenga kuviunganisha vijiji vyote vya Zanzibar na usafiri wa kisasa.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Nassor Shaaban, ameeleza kuwa zaidi ya Sh. bilioni 700 zimeingizwa sokoni na mfuko huo ili kuimarisha uchumi. Alisema pia Sh. bilioni 250 zimelipwa kwa wastaafu ndani ya miaka minne ya awamu ya nane na wastaafu 15,000 wanaendelea kulipwa pensheni kwa mafanikio kila mwezi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitembelea mradi wa nyumba 370 zinazojengwa katika eneo la Bumbwini Kidazini, Mkoa wa Kaskazini Unguja baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo, ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar juzi. Kulia kwa kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mattar Zahor Masoud na kushoto ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohammed. **PICHA: IKULU**

# Askofu: Walimu wasitelekezewe mzigo wa malezi

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Mara, Dk. George Okoth, amewataka wazazi kuacha tabia ya kuwatelekezea walimu mzigo wa malezi ya watoto wao bali kuwekeza kwao malezi bora ili kuandaa taifa lenye maadili.

Askofu Okoth alitoa kauli hiyo juzi, akiwahubiria waamini wa kanisa hilo katika ibada maalumu ya kumbukumbu ya tohara na kubatizwa kwa Yesu Kristo. "Wazazi wa kisasa wametingwa sana na shughuli za maendeleo yao wanafanya kazi, kwa hiyo basi jukumu la malezi ya watoto wamewasukumia walimu peke yao wanasahau kuwa ili mtoto aweze kukua ni lazima mwalimu afanye kazi yake na mzazi afanye jukumu lake la malezi ili mtoto awe raia mwema," alisema. Aidha, alisema watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu, mambo muhimu ya kuwarithisha ni pamoja na elimu dunia na kumjua Mungu.

Aliwataka wazazi kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha wanalea watoto wao kwa kuwa ni haki yao kupata malezi bora ili kuwaokoa katika matendo maovu yasiyoipendeza jamii na Mungu kwa ujumla.

Askofu Okoth, aliwakumbusha waamini wa kanisa hilo kukumbuka kumuomba Mungu awaongoze vyema katika kuita watoto majina yenye uhalisia wa malengo wanayotaka yatokee kwenye maisha yao.

Naye Mchungaji Baraka Ogina alisema, kanisa hilo limekuwa na desturi ya kuwahudumia watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu kwa kuwakusanya pamoja kila Jumamosi na kuwapa mahitaji ya msingi ya chakula na mavazi.

"Tuna kituo cha huduma ya mtoto maarufu (Compassion) tuna watoto zaidi ya 250 ambao tuliwakusanya kwenye mitaa ya Manispaa ya Musoma kila Jumamosi wanakuja mafundisho na wanapata chakula cha asubuhi, mchana na jioni wanarudi kwenye familia zao." Aliiambia Nipashe kuwa mafundisho wanayotoa kwa watoto hao ni neno la Mungu na elimu ya jamii na baadhi ya watoto wamesaidiwa kusoma elimu ya msingi, sekondari vyuo vikuu, vyuo vya kati na wengine wamepelekwa katika vyuo mbalimbali vya ufundi.

# SHAMRASHAMRA ZA UFUNGUZI WA KITUO CHA MABASI ZANZIBAR




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika hafla ya ufunguzi wa kituo cha kisasa cha mabasi Kijangwani Wilaya ya Mjini Unguja jana.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kuzindua kituo hicho, jana mjini Zanzibar.



Mwonekano wa jengo la kituo cha kisasa cha mabasi Kijangwani Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar kilichofunguliwa jana.




Wananchi  wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na wageni waalikwa wakiwa na mabango yenye mchoro wa picha ya Rais wa Zanzibar.



Wananchi wakifuatilia hotuba ya Rais.




Wananchi wakimsikiliza Rais wakati wa ufunguzi wa kituo hicho. **PICHA: ZOTE IKULU**

# Mara yaainisha maeneo saba kukuza uchumi

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Musoma mkoani Mara, imeainisha maeneo saba ya uwekezaji ukiwamo uvuvi wa vizimba unaohusisha viwanda vya kuchakata minofu ya samaki ili kusaidia kukuza uchumi wa wilaya hiyo.

Maeneo mengine yanayotajwa ni kilimo cha umwagiliaji, kikiambatana na viwanda vya usindikaji mazao, kiwanda kipya cha nguo na utalii katika visiwa ndani ya Ziwa Victoria.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Chikoka ametaja maeneo mengine kuwa ni uchimbaji madini ya dhahabu na gesi, ufugaji na kuwa na kiwanda cha kisasa cha kusindika maziwa.

Alisema hayo hivi karibuni, kwenye kongamano la fursa za kukuza uchumi na maendeleo ya wilaya yake na kuongeza eneo lingine la uwekezaji kuwa ni katika elimu bora na ya ufundi.

"Tuna fursa hizo za kuinua za kukuza uchumi na maendeleo yetu, hivyo wadau wote wa maendeleo wilaya hii tunashirikiana kuhakikisha tunatumia fursa zilizopo kuinua uchumi wetu," alisema Chikoka.

Aidha, kupitia maeneo hayo ya uwekezaji itakuwa ni rahisi kuongeza kasi ya ajira mpya kwa vijana wa wilaya hiyo na kuwasaidia kuwa na maisha ya bora zaidi.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuchangamkia mipoko inayotolewa na halmashauri na kuitumia katika uwekezaji wa uvuvi wa kutumia vizimba na kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Bugwema na Suguti.

Prof. Muhongo alisema uvuvi wa vizimba unafanyika maeneo mbalimbali duniani na una matokeo mazuri, hauna madhara kwa samaki wadogo na kuwataka wananchi wauchangamkie.

Aidha, anatamani jimboni kwake kuwa na viwanda vidogo vya kusindika samaki na vya kukausha dagaa ili isichukue muda mrefu kuwakausha kwa njia ya kienyeji na kusababisha usafirishaji kwenda sokoni kuchelewa.

"Lakini pia tujikite katika kilimo cha pamba na alizeti na kuweka viwanda vya usindikaji wa mafuta ya kula yanayotokana na mazao hayo. Vilevile tunatakiwa kuwa na kiwanda cha kisasa cha nguo, sio kufufua Mutex kwani hicho kimeshachakaa," alisema Prof. Muhongo.

Alionesha fursa za kiuchumi zilizomo wilayani humo ambazo zikitumika vizuri zinaweza kubadilisha maisha ya wananchi kwa kujiletea maendeleo wanayotaka.

"Hivyo, wito wangu ni huo ambao nimeutoa kwa wananchi, wadau wa maendeleo na serikali, ninaamini ukitekelezwa unaweza kuwa na matokeo mazuri," alisema.

# 'Wapambe chanzo mnyukano Lissu, Mbowe'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Victoria na mgombea wa Makamu Mwenyekiti Taifa, Ezekia Wenje, amesema wapambe wa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe na makamu wake (Bara), Tundu Lissu, ndio chanzo cha mnyukano ndani ya chama hicho.

Aidha, amesema endapo wanachama watamchagua Lissu kuwa mwenyekiti atatafuta namna ya kufanya naye kazi ili kuhakikisha wanakijenga chama hicho.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mwanza kuhusu nia yake ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho taifa.

Alisema minyukano inayoendelea ndani ya CHADEMA inasababishwa na wapambe wa viongozi hao ambao kila upande unatukana upande mwingine.

"Lazima chama kiwe tested (kijaribiwe). Wanaoleta shida ni wapambe wa Mbowe na Lissu, hautasikia Mbowe amemtukana Lissu wala Lissu amemtukana Mbowe," alisema Wenje.

Wenje alisema pamoja na minyukano ya wapambe, Mbowe na Lissu hawana tofauti kati yao.

Alisema ili chama kisiwe tegemezi kwa mtu au watu fulani, atasisitiza na kumshauri mwenyekiti atakayekuwapo waongeze nguvu katika suala la Chadema Digital, ambayo itahakikisha kila mwanachama na viongozi wanalipia ada ili chama kiendeshe shughuli zake.

Kauli hiyo ya Wenje imewaibua mashabiki wa viongozi hao ambao wamemshambulia mitandaoni, kwa kudai kuwa na yeye (Wenje), ni miongoni mwa wapambe wanaosababisha mnyukano ndani ya CHADEMA.

Kuhusu kufanyakazi na Lissu ikiwa atashinda uenyekiti wa CHADEMA Taifa, alisema: "Yaani wanachama wamchague, mimi ninanuna vipi kwa mfano. Lazima niangalie namna gani tutatengeneza mahusiano ya kufanya kazi pamoja."

Aidha, alisema anamheshimu Lissu na ni ndugu yake wa karibu tangu wamekutana na mchakato wa siasa uliopo kwa sasa haiwezi kuwatenganisha hata siku mmoja.

"Nipo tayari kuwa msaidizi wa mwenyekiti yeyote atakaye chaguliwa na wanaChadema ili tukijenge chama chetu katika misingi imara," alisema Wenje.

"Mimi na Lissu ni 'best friend', mke wangu na wake ni marafiki sana na tumekuwa tukitembeleana akija kwangu namchinjia ng'ombe nimehangaika kipindi ameshambuliwa kwa risasi na sisi tupo sawa na kipindi hiki kitaisha na mambo mengine yataendelea," alisema.

Aidha, aliwataka wafuasi wake kutumia kauli za staha katika kujenga hoja na sio matusi kwa kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi huo.

"Tafadhali wale wanaotukana viongozi na wagombea wekeni akiba ya maneno kuna maisha baada ya Januari, 21. Na hata kama unaniunga mkono mimi usitukane mwingine," alisisitiza Wenje.

Kadhalika, alisema chama hicho kwa wakati huu kinapitia mchakato mkali na kuwa kama kinachotaka kuchukua dola lazima kijaribiwe na kuvuka kwake katika jaribu hilo kitakuwa imara maradufu.

Alisema kwa sasa chama hicho hakihitaji tena mwamba mmoja wa kukivusha bali kinahitaji muunganiko wa pamoja wa viongozi pamoja na wanachama kuhakikisha kinavuka hatua moja kwenda nyingine.

Kadhalika, alisema kama alivyosimama katika majukumu mbalimbali aliyoyatumikia kwenye chama hicho kwa nyakati tofauti atahakikisha anatekeleza wajibu wake wa kikatiba ikiwa ni pamoja na kumshauri mwenyekiti pamoja na kudhibiti hali ya maadili ndani ya chama.

Mbowe na Lissu wametangaza kugombea uenyekiti wa chama hicho taifa, katika uchaguzi utakaofanyika Januari 21, 2025.



Dereva wa basi la Kisire linalofanya safari zake kati ya Mwanza na Sirari mkoani Mara, Adam Charles (30), akiongozwa na askari wa Jeshi la Polisi kuelekea katika Mahakama ya Wilaya ya Magu jana ambako alisomewa mashtaka 22 ikiwamo kusababisha majeruhi kwa abiria na uharibifu wa mali. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Kamati za Bunge kujifungia siku 18 Dodoma

**Na Jenifer Gilla**

KAMATI za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinatarajia kujifungia Dodoma kwa siku 18 kwa shughuli maalum ikiwamo kuchambua miswada ya sheria.

Kamati hizo pia zitachambua sheria ndogo, kupokea taarifa za utendaji wa serikali na taasisi zake, kuchambua taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma jana, ilisema kuwa vikao hivyo vinatarajiwa kuanza Januari 6 hadi 24, mwaka huu vikifuatiwa na mkutano wa 18 wa Bunge unaotarajiwa kuanza Januari 28, mwaka huu.

Taarifa hiyo ilitaja kamati zitakazoanza kufanya vikao hivyo kuwa ni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Januari 6 na kamati nyingine zitafuata Januari 13.

Aidha, ilieleza kuwa kamati mbili zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Wizara, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2023. Ilisema Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itapokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma kuangazia kama ili uwekezaji wake umezingatia taratibu na miongozo ya biashara.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo itachambua Sheria Ndogo.

Ilisema pia Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Maji na Mazingira na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) zitachambua miswada ya sheria.

Ilisema pia kamati 11 za kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Serikali na Taasisi zake.

Aidha, Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2024.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila la heri Simba SC, Yanga vita kutinga robo fainali CAF

**VIGOGO** wa soka nchini, Simba na Yanga zote za Dar es Salaam ndio timu wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao wanashiriki hatua ya makundi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati, Simba 'Mnyama' wenyewe wanapeperusha bendera ya Tanzania katika hatua hiyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga iliyoko Kundi A inaburuza mkia baada ya kuvuna pointi moja baada ya kucheza mechi tatu za hatua ya makundi, na leo itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuwakaribisha TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Mechi ya leo kwa Yanga ni muhimu sana kwa sababu inahitaji kuzibakisha pointi zote tatu ili kurejesha matumaini ya kusonga mbele katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka, matokeo chanya pekee ndio yatawafanya warejeshe nguvu ya kupambana kwenye michezo iliyobakia ya hatua hiyo ya makundi.

Endapo Yanga itapata ushindi, mechi zake mbili zitakazobakia pia zitakuwa ni za maamuzi na si za kucheza ili kukamilisha ratiba kutoka kwa Al Hilal ya Sudan yenye pointi tisa, tayari kuweka mguu mmoja ndani katika hatua ya robo fainali.

Na kwa upande wa Simba ambayo pia iko Kundi A, na kwenye msimamo iko katika nafasi ya tatu, ikiwa na pointi sita sawa na Bravos do Maquis ya Angola na CS Constantine, zikitofautiana idadi ya mabao ya kufunga na kufungwa, inahitaji ushindi ili kujiimarisha kwenye msimamo wa kundi hilo.

Simba itakuwa ugenini, hilo si tatizo kwa sababu endapo watacheza karata zao vyema, basi wanaweza kupata ushindi au kuambulia sare, kikubwa ni wachezaji kujituma, kuongeza umakini na kutowadharau wapinzani wao kwa kuangalia matokeo ya mchezo uliopita.

Haijalishi Mnyama kesho anacheza ugenini, tena kwenye ardhi ya Mwarabu, katika mpira lolote linaweza kutokea kama wachezaji wataingia kwa kuuona mchezo huo ni wa fainali na wanachotakiwa kukifanya ni kushinda ili kurejea na kikombe nyumbani.

Kufanya vizuri kwa vigogo hao, sio tu kutaipa heshima Tanzania, lakini wataendelea kujihakikisha kutoa wawakilishi wanne katika mashindano yajayo ya CAF, kama Algeria, Misri na Morocco ambao hiyo imekuwa ni kawaida kwao.

Ili kuhakikisha wanajipanga vyema, bado makocha wanayo nafasi ya kuimarisha vikosi vyao kwa kufanya usajili ambao utawafikisha kwenye malengo yao, klabu zinatakiwa kutumia dirisha hili la usajili kuwanasa nyota wanaoendana na hatua ambazo wanataka kufika.

Tunawakumbusha viongozi wa Simba na Yanga kuacha kusajili wachezaji ambao wanahitaji kupata muda ili wawe wazoefu, ongezeni 'silaha' ambazo ziko tayari kuingia katika mapambano, isiwe wanaangalia washindani wao katika Ligi Kuu Tanzania Bara pekee, wasajili wachezaji wenye uwezo wa kuhimili mikikimikiki dhidi ya klabu nyingine kongwe za Afrika.

Umefika wakati wa Simba na Yanga sasa kuweka malengo ya kutwaa taji la Afrika la Kombe la Shirikisho au Ligi ya Mabingwa na si kupambana kucheza robo fainali au nusu fainali. Ndoto kubwa ya mashabiki na wadau wa michezo nchini ni kushuhudia moja ya taji hilo la CAF linatua katika ardhi ya Tanzania.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wachezaji wa Simba na Yanga kuwakabili wapinzani wao kwa tahadhari na kutowadharau, wakumbuke hakuna timu iliyofika hatua ya makundi inahitaji kusindikiza wengine, kila timu inahitaji kuweka historia.

Kusonga mbele katika mashindano hayo mawili, sio tu kutalitangaza vyema jina la Tanzania kimataifa, lakini itaendelea kumpa heshima Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa shabiki namba moja wa michezo nchini.

Kwa hapa nyumbani, huu ni wakati muhimu wa mashabiki wa soka bila kujali itikadi, kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuishangilia Yanga, shabiki ni mchezaji wa 12, kama ambavyo tunashuhudia mechi za dabi zinajaa au Tamasha la Wiki ya Mwananchi, leo ni siku nyingine muhimu kwenda kuwapa hamasa wachezaji ili kupata pointi tatu.

Mungu ibariki Simba na Yanga, katika vita ya kusaka tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano ya CAF katika ngazi ya klabu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Mapinduzi Cup iwe chachu ya kupata 'silaha' za CHAN

**MASHINDANO** ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi mwaka huu yameanza kufanyika kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba, Zanzibar jana kwa 'wanandugu' Timu ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), ilipowakaribisha Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars).

Michuano hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Timu ya Taifa ya Burkina Faso itakapocheza dhidi ya Harambee Stars ya Kenya, michezo yote ikipigwa, saa 20:15, usiku.

Fainali ya michuano hiyo itafanyika Januari 13, mwaka huu kwenye uwanja huo huo wa Gombani.

Kumekuwa na tofauti kidogo kwenye michuano hiyo msimu huu. Badala ya klabu kuchuana, sasa imezishirikisha timu za taifa.

Sababu inaeleweka. Kumekuwa na mwingiliano wa ratiba hasa kwa timu za Simba na Yanga ambazo ni washiriki 'wakubwa' wa michuano hiyo, wamebanwa na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Ikumbwe michuano ya kimataifa imeanza mapema sana msimu huu kutokana na ifikapo Februari, mwaka huu kuna Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazopigwa hapa nchini, Kenya na Uganda.

Pamoja na mengine, waandaaji wa michuano hiyo wakaona wabadilishe mfumo, badala ya timu za klabu basi zicheze timu za taifa.

Timu zilizothibitisha kushiriki mashindano hayo ni nne, wenyeji Zanzibar, Tanzania Bara, Burkina Faso na Kenya, ambazo tayari zipo visiwani kwa ajili ya kuanza kupambana kuwania kombe hilo.

Tunaipongeza kamati ya maandalizi ambayo haikuona sababu yoyote ya kuahirishwa michuano hiyo licha ya changamoto zote hizo.

Tumeona wachezaji waliochaguliwa kwa pande zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar wengi wao ni vijana ambao bado wana safari ndefu katika soka la nchi hii.

Kamati ya Ufundi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) na Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Stars, Ahmad Ally, amejitahidi sana kuchagua wachezaji vijana kutoka Serengeti Boys (U-17), Ngorongoro Heroes (U-20), pamoja na wale ambao waliokuwa wanaitwa kwenye kikosi cha Taifa Stars lakini hawapati namba.

Wamekuwa hawapati nafasi ya kucheza mbele ya wachezaji kama Mbwana Samatta, Simon Msuva na baadhi wanaocheza soka la kulipwa nje ya Tanzania.

Ukiacha wachezaji wa Simba, Yanga na Azam, ambao baadhi yao wanaitwa ama kwa mazoea, au viwango wanavyoonyesha kwenye Ligi Kuu na michuano ya kimataifa, michuano hii itasaidia mno kutazama wachezaji kutoka timu nyingine ambazo wamekuwa hawaonekani au kutazamwa sana na mashabiki.

Bara na Zanzibar kwa sasa zina wachezaji ambao hawatokani na Simba na Yanga, hivyo ni fursa sasa ya wachezaji wenyewe kuonyesha walichonacho ili kuondoa dhana timu hizo ndizo zinazotoa nyota wenye ubora.

Tumeona kuna wachezaji wengi kutoka timu za Ligi Kuu Bara, na Zanzibar, sasa hii ni fursa kwao kwa sababu ni jukwaa la kuteuliwa kuunda kikosi cha CHAN.

Kocha Ahmed, amekiri mchezaji atakayefanya vyema katika michuano hii, ana uwezekano mkubwa wa kuwamo katika kikosi cha CHAN ambacho nadhani kitatajwa hivi karibuni.

Wakipatikana kutoka Zanzibar, halafu wengine Bara, na baadhi waje kuongezwa kutoka Simba na Yanga, nadhani tunaweza kupata kikosi bora.

Hata hivyo ni lazima kwanza wachezaji wenyewe walioitwa kufanya kazi ambayo kila mmoja ataona ni kweli wanastahili kuitwa.

Bahati nzuri kwenye vikosi vyote hivi viwili, hakuna wachezaji kutoka nje ya nchi, wala Simba na Yanga, hivyo hakuna visingizio, kazi kwao.

## Mbunge aombwa akumbukwe anapochangia miradi

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

MBUNGE wa Jimbo la Mpanda mjini, Sebastian Kapufi amewataka watendaji wa serikali wapoandaa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo wasiishie kumshukuru Rais pekee kwa kupeleka fedha za miradi hiyo bali wamkumbuke na yeye.

Alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo aliyoifanya katika kata zilizopo kwenye Jimbo la Mpanda mjini.

"Mwalimu nashukuru tunamshukuru Mama Samia... kwa kutuletea fedha, ukimshukuru hata na mbunge wala hukosei kwa kuwa ndio napiga kelele kwenye Bunge kule bajeti ije huku.

Kwa hiyo mnapoandika haya mavitu msisahau kutaja na hilo...kwa hiyo bila sisi kukaa kule kupitisha bajeti hamuioni mia huku...kwa hiyo ni mchakato," alisema.

Alisema anapeleka shukrani kwa kila mmoja kutokana na jitihada zake ndio maana miradi inakamilika na manufaa yanaonekana kwa wananchi ambao ndio walengwa wakuu.

Kauli ya Mbunge Kapufi imekuja baada ya kuona katika maeneo mengi, kama ilivyo Shule ya Sekondari Kapalakangao iliyopo Kata ya Kazima kukagua miradi ya maendeleo jitihada zake hazitajwi.

Awali, katika Shule ya Sekondari Kapalakangao, Mkuu wa shule hiyo, Mario Mhagama katika taarifa yake ya utekelezaji wa mradi wa nyumba pacha za walimu walipokea zaidi ya Sh. milioni 110.

Alisema katika shule kuna changamoto kadhaa ikiwamo ya upungufu wa walimu na ukosefu wa nishati ya umeme na walimwomba mbunge awasaidie, lakini hawakutambua mchango wake wa kupigania maendeleo ya kielimu katika jimbo hilo.

Mbunge huyo alichangia Shilingi milioni saba kutoka mfuko wa jimbo ikiwa ni kwa ajili ya kutatua changamoto ya ukosefu wa nishati ya umeme.

# Dereva basi kizimbani, asomewa mashtaka 22

**Na Vitus Audax,** MWANZA

DEREVA wa basi la abiria la Kisire linalofanya safari zake kati ya Mwanza na Sirari mkoani Mara, Adam Charles (30), amepandishwa kizimbani na kusomewa shtaka moja lenye makosa 22 ikiwamo kusababisha majeruhi kwa abiria na uharibifu wa mali.

Charles alipandishwa kizimbani jana na kusomewa shauri hilo la usalama barabarani katika Mahakama ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Erick Kimaro.

Akisoma shtaka hilo mbele ya Hakimu Kimaro, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nuru Nko, alidai kuwa mshtakiwa anakabiliwa na kosa la uharibifu wa mali ambayo ni basi alilokuwa akiendesha namba T. 229 DST.

Nko alidai mahakamani hapo kuwa mshtakiwa wakati akiendesha basi la Kampuni ya Kisire Desemba 19, 2024, alisababisha ajali eneo la Kisamba wilayani Magu, mkoani humo na kusababisha majeruhi kwa abiria 21.

Alisema mshtakiwa huyo ambaye ni Mkazi wa National, jijini Mwanza alikuwa akiendesha gari kwa mwendokasi na bila umakini uliosababisha ajali na majeraha.

Alidai kitendo cha kusababisha majeraha hayo kwa abiria ni kinyume na sheria.

Hata hivyo mshtakiwa huyo alikana kutenda makosa hayo.

Mwendesha Mashtaka Nko alidai mahakamani kuwa upelelezi umekamilika na kuomba ipangwe tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali na kupeleka mashahidi.

Baada ya hoja hizo, Hakimu Mkazi Mkuu wa mahakama hiyo, Erick Kimaro, aliruhusu dhamana kwa mshtakiwa akimtaka kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho wa Serikali ya Mtaa.

Pia, Hakimu Kimaro alisema wadhamini hao wanapaswa kusaini dhamana ya maneno ya Shilingi milioni tatu na kuwa na kitambulisho kinachotambulika.

Mshtakiwa alishindwa kukidhi masharti ya dhamana kutokana na kuwa na mdhamini mmoja pekee ambaye naye hakuwa na barua ya utambulisho iliyokidhi masharti hayo pamoja na kitambulisho.

Hakimu Kimaro aliahirisha shauri hilo hadi Januari 16, litakapoitwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali ya shtaka linalomkabili.




Baadhi ya wazazi na watoto wakinunua madaftari ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuingia kwenye masomo katika mwaka 2025. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH.**

# Mbaroni tuhuma utapeli wizi kimtandao

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATUHUMIWA Karim Abdallah (20) na Joseph Mbaraka (27), wote wakazi Mtaa wa Kihonjo wametiwa mbaroni kwa kujihusisha na utapeli kwa njia ya mtandao maarufu 'Halo Halo' katika Wilaya ya Kilombero, mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Desemba 31, 2024 katika mtaa wa Kihonjo, Kata na Tarafa ya Ifakara, wilayani humo.

Alisema walikamatwa baada ya kuwekewa mtego na makachero wa polisi na baada ya kupewa taarifa ya kutaka kutapeli wananchi na walikutwa wakiwa na laini mbalimbali za simu ambazo zimesajiliwa wa majina tofauti na ya kwao.

Mkama alisema watuhumiwa hao walikuwa wakizitumia laini hizo kwa kutuma ujumbe mbalimbali kwa wananchi kwa minajiri ya kuomba kiasi cha fedha kwa njia ya ulaghai. Kamanda wa polisi wa mkoa huo alisema matukio ya utapeli kwa njia ya mtandao yamekithiri zaidi katika maeneo ya mji wa Ifakara wilayani Kilombero, mji wa Turiani wilayani Mvomero na mji wa Rudewa, Wilaya ya Kilosa.

Mkama alisema sababu kubwa ya kukithiri wa matukio hayo ni kutokana kuwapo kwa mzunguko mkubwa wa fedha pamoja na shughuli za kilimo na kwamba utapeli huo unatokea zaidi kipindi cha mauzo ikiwa na tamaa ya watu kutaka kupata fedha kwa haraka.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani Morogoro linamshikilia Musa Kidumla (28), mkulima na mkazi wa kitongoji cha Melela Mlandizi, Kata ya Mangae, Tarafa ya Mlali, Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro kwa tuhuma za kukutwa akiwa na kiasi kikubwa cha mafuta yenye vinasaba vya mlipuko.

Mafuta hayo ambao yanadhaniwa ni aina ya dizeli na petroli yaliyokuwa yamehifadhiwa kwenye mapipa kumi sawa na ujazo wa lita 2,000.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Alex Mkama, alisema ya kwamba mtuhumiwa huyo alikamatwa Desemba 29, 2024 majira ya jioni katika kitongoji cha Melela Mlandizi, Kata ya Mangae, wakati askari polisi wakiwa kwenye doria.

Pia, yalikamatwa madumu 93 yenye ujazo wa lita 20 ya petroli yanayokadiriwa kuwa na ujazo wa lita 1,860, ndoo tatu za kukingia mafuta zikiwa ndani ya gari lenye namba za usajili T. 897 CUT aina ya Noah.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo alisema uchunguzi umebaini kuwa mtuhumiwa anatumia mbinu ya kuongea na madereva wanaosafirisha mafuta na mizigo mingine kula nao njama na kuiba mafuta kisha kuhifadhi ndani ya nyumba kwa ajili ya kufanya biashara ya kuuza mafuta hayo bila kuwa na leseni.

"Kwa sasa tupo katika hatua ya kumfuatilia mmiliki wa gari hiyo na pia kuendelea na msako maalum katika kuzuia matukio ya moto unaoweza kusababishwa na hawa wauza mafuta, kimsingi maeneo ya makazi ya watu hayaruhusiwa kufanya hizo shughuli za kuuza mafuta," alisema Mkama.

Alisema, uchunguzi unakamilishwa kwa haraka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na vyombo vingine vya dola ili hatua za kisheria ziweza kuchukuliwa kwa wahusika wote watakaobainika.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Wenje: Lissu akiwa mwenyekiti nitafanyakazi naye

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Victoria na mgombea wa Makamu Mwenyekiti Taifa, Ezekia Wenje, amesema endapo wanachama watamchagua Tundu Lissu kuwa mwenyekiti atalazimika kutafuta namna ya kufanya naye kazi ili kuhakikisha wanakijenga chama hicho.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mwanza kuhusu nia yake ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho taifa.

"Yaani wanachama wamchague, mimi ninanuna vipi kwa mfano. Lazima niangalie namna gani tutatengeneza mahusiano ya kufanya kazi pamoja," alisema Wenje.

Aidha, alisema anamheshimu sana Lissu na ni ndugu yake wa karibu tangu wamekutana na mchakato wa siasa uliopo kwa sasa haiwezi kuwatenganisha hata siku mmoja.

"Nipo tayari kuwa msaidizi wa mwenyekiti yeyote atakaye chaguliwa na wana-Chadema ili kukijenge chama chetu katika misingi imara."

"Mimi na Lissu ni 'best friend', mke wangu na wake ni marafiki sana na tumekuwa tukitembeleana akija kwangu namchinjia ng'ombe nimehangaika kipindi ameshambuliwa kwa risasi na sisi tupo sawa na kipindi hiki kitaisha na mambo mengine yataendelea," alisema.

Aidha, aliwataka wafuasi wake kutumia kauli za staha katika kujenga hoja na sio matusi kwa kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi huo.

"Tafadhali wale wanaotukana viongozi na wagombea wekeni akiba ya maneno kuna maisha baada ya Januari, 21. Na hata kama unaniunga mkono mimi usitukane mwingine," alisisitiza Wenje.

Kadhalika, alisema chama hicho kwa wakati huu kinapitia mchakato mkali na kuwa kama kinachotaka kuchukua dola lazima kijaribiwe na kuvuka kwake katika jaribu hilo kitakuwa imara maradufu.

Alisema kwa sasa chama hicho hakihitaji tena mwamba mmoja wa kukivusha bali kinahitaji muunganiko wa pamoja wa viongozi pamoja na wanachama kuhakikisha kinavuka hatua moja kwenda nyingine. Kadhalika, alisema kama alivyosimama katika majukumu mbalimbali aliyoyatumikia kwenye chama hicho kwa nyakati tofauti atahakikisha anatekeleza wajibu wake wa kikatiba ikiwa ni pamoja na kumshauri mwenyekiti pamoja na kudhibiti hali ya maadili ndani ya chama.

Kuhusu mtifuano uliopo baina ya miamba wawili wa chama hicho wanaowania nafasi ya mwenyekiti, Wenje alisema kelele zote zinasababishwa na wapambe, lakini viongozi hao hawana tofauti yoyote.

Aidha, alisema ili chama kisiwe tegemezi kwa mtu au watu fulani atasisitiza na kumshauri mwenyekiti atakayekuwapo waongeze nguvu katika suala la Chadema Digital ambayo itahakikisha kila mwanachama na viongozi wanalipia ada ili chama kiendeshe shughuli zake.

# LATRA yakamata magari 20 kutoza nauli kubwa

**Na Benny Kingson,** TABORA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Tabora, imeyakamata magari 20 yanayofanya safari kutoka Tabora mjini kwenda wilayani Sikonge kwa kutoza abiria nauli kubwa kupita kiwango kinachotakiwa kisheria kwa madai ya gharama za uendeshaji kuongezeka.

Ofisa Mfawidhi LATRA, Mkoa wa Tabora, Nelson Mmari, akitoa taarifa kwa gazeti hili alisema kuwa magari hayo wameyakamata kutokana na ukaguzi walioufanya na kubaini yanatoza nauli kati ya Sh. 4,000 hadi Sh. 5,000 badala ya Sh. 3,700 inayotambulika kisheria.

Mmari alisema kuwa katika ukaguzi huo wamegundua wahusika wa magari hayo wamekuwa hawarudishi chenji kwa abiria wanapotoa pesa ili kulipa nauli na kwamba wamekuwa hawawapi tiketi zinazoonesha malipo halisi.

"Serikali ilitangaza nauli halali Desemba mwaka 2023 na kuanza kutumika nchi nzima na mkoani Tabora tulimwambia Mkuu wa Mkoa ambaye aliwaita wadau wote wa usafirishaji na kuwaeleza na kuwahimiza kufuata sheria zote za umiliki wa vyombo vyao," alisema.

**"Serikali ilitangaza nauli halali Desemba mwaka 2023 na kuanza kutumika nchi nzima na mkoani Tabora tulimwambia Mkuu wa Mkoa ambaye aliwaita wadau...**

Alisema kuna magari kati ya 50 hadi 70 yanayotoa huduma ya usafirishaji toka Tabora mjini kwenda wilayani Sikonge na kuna umbali wa kilomita 77 na kama wamiliki wa magari watafuata sheria zilizopo na kuwafuatilia watu waliowaweka kusimamia magari yao watapata faida kubwa zaidi. Ofisa mfawidhi huyo alisema kuwa magari yote yanayofanya shughuli za usafirishaji yanatakiwa kuwa na mkanda wenye rangi yake kulingana na uelekeo waliopangiwa kwa magari yanaenda wilayani Sikonge yanatakiwa kuwa na mkanda wa rangi ya kijani na ubavuni kuandikwe nauli inayotakiwa pamoja na eneo linapotoka na kuelekea.

"Magari yote yanatakiwa kuwa na tiketi, yale makubwa watoe tiketi za kielektroniki na haya ya wilayani yanatakiwa kutoa tiketi zinazoonesha namba za gari, jina la kampuni, jina la abiria, siti yake na kiwango cha nauli na hii inasaidia kuonesha nauli halali inayotozwa, kulitambulisha gari na kumtambulisha abiria alipotoka na anapokwenda," alisema. Alisisitiza kuwa wamiliki na madereva wa magari wasisingizie kupanda au kushuka kwa gharama za mafuta ili kupandisha nauli na kwamba gharama za uendeshaji sio mafuta pekee ni pamoja na vipuli na malipo ya wafanyakazi na mambo mengine ambayo ni ya kawaida," alisema.

Mmari aliwataka kufuata sheria za usafirishaji kwa kuvaa sare za kaunda suti za rangi ya bluu ama tisheti zenye nembo ya kampuni, kutoza nauli halali na kutoa tiketi za kieletroniki na wanatoa tiketi za kawaida wahakikishe zinakuwa vigezo vyote na watambue serikali ndio yenye mamlaka ya kutangaza mabadiliko ya nauli.

Aidha, aliwataka wamiliki wa magari kutotumia wapigadebe ama vishoka kuwakatia tiketia abiria kwa kuwa wanawaumiza na ni kinyume cha sheria na kwamba wanawaongezea gharama za uendeshaji kwa kupigwa faini watakapobainika na kukamatwa na watu hao wanajinufaisha kupitia mali zao.

Alisema mabasi yapo ya kutosha, hakuna tatizo la upungufu na kwamba abiria wahakikishe wanalipa nauli zao wanapoona basi husika lipo kituoni na wapande na kuingia ndani ili wahudumiwe kwa kulipa nauli zao halali nakupatiwa tiketi halisi.




Mgombea nafasi ya uenyekiti wa Baraza la Wanawake-BAWACHA, Sharifa Suleiman (wa tatu kushoto), akiwa katika maandamano eneo la Biafra wakati anarudisha fomu katika ofisi za CHADEMA Kanda ya Pwani, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wakaguzi TBS kutambulika kimataifa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKAGUZI wa vituo 18 vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), vilivyopo nchini sasa watakuwa wanatambulika kimataifa na kuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi popote duniani baada ya kupewa mafunzo yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia katika udhibiti wa bidhaa zenye ubora unaokubalika.

Maabara 18 za TBS nazo zina uwezo wa kufanya ukaguzi wa viwango vinavyotambulika kimataifa na kudhibiti kuingia na kutoka kwa bidhaa nchini.

Hatua hiyo inatokana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), kutoa vifaa vya kisasa vya ukaguzi na maabara vyenye uwezo wa kufanya kaguzi za viwango vya kitaifa na kimataifa pamoja na kutoa mafunzo ya mbinu za kisasa kwa wakaguzi 180 ambao watatambulika kimataifa kwa kufanya kaguzi hizo duniani.

Mradi unaofahamika kama Qualitan chini ya mpango wa Begin unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) pia utaboresha shughuli za michakato usanifishaji, miundombinu ya Tehama na usimamizi wa mifumo ya taarifa.

Mratibu wa kitaifa wa mradi wa Qualitan kutoka UNIDO, Valency Mutakyamirwa, alisema hayo katika ufungaji wa mafunzo ya wakaguzi 180 yaliyolenga utekelezaji wa kiwango cha ISO17020 na matumizi ya mbinu za ukaguzi kwa kuzingatia tathmini ya hatari.

Mutakyamirwa, alisema mradi huo utasaidia pia wajasiriamali wadogo na wa kati kufikia viwango vya kufuata taratibu ili kupunguza gharama za kufuata viwango na kuboresha upatikanaji wa masoko pamoja.

Alisema UNIDO inaamini kuwa mradi huo wa Qualitan utachangia katika kuboresha mfumo wa ubora wa nchi hatimaye kuongeza fursa kwa wateja wa TBS hasa wajasiriamali wadogo na wa kati katika kupanua wigo wa masoko na uaminifu katika bidhaa zao katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Naye Meneja wa Ukaguzi na Uzingatiaji wa Sheria wa TBS, Nuru Mwasulama, alisema limeendelea kuwa ni chombo muhimu na imara cha ukaguzi wa bidhaa nchini ili kuwalinda walaji.

Mwasulama alisema TBS ilianza kujengewa uwezo na kwa wataalamu wake kuanzia Julai 2023 na makundi manne yamefundishwa na kufanya jumla yao kufikia washiriki 180.

Mwasulama alisema kuwa mkaguzi ni askari wa kwanza wa wananchi wa Tanzania kulinda kwa maana anahusika kufanya uamuzi wa udhibitishaji wa ubora wa bidhaa.

Naye Ofisa Udhibiti Ubora wa Shirika hilo kitengo cha upokeaji wa bidhaa Bandari ya Dar es Salaam, Salome Makelemo, akiongea kwa niaba ya washiriki wenzake alisema mafunzo hayo yameleta tija kwao kwa kuongeza maarifa kwenye ukaguzi katika nyanja mbalimbali za kimataifa.

Makelemo alisema mafunzo hayo yametolewa wakati mwafaka unaoendana na mabadiliko ya kiteknolojia ya kidigitali kwa kutumia maabara za kidijitali ambazo majibu yanafika kwa mlaji kwa uharaka.

Alisema licha ya wimbi kubwa la ujasiriamali unaojitokeza wa uanzishwaji viwanda vidogo wao TBS wanalo jukumu kubwa la kuendelea kuwapa elimu na mafunzo ili bidhaa wanazozalisha zikidhi viwango bora kwa ajili ya kulinda mlaji.



HABARI DODOMA

# Askofu Mangwela awataka waamini kutunza mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Evangelist Assembly of God Tanzania (EAGT) Jimbo la Dodoma, Robert Mangwela, amewataka Watanzania kuweka vipaumbele kwenye utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti ili kukabilina na athari za mabadiliko tabianchi.

Askofu huyo ambaye kwa sasa ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la New Jerusalem Ihumwa jijini hapa, alitoa rai hiyo wakati akizungumza muda mfupi baada ya kumalizika ibada ya kuukaribisha mwaka 2025 iliyofuatiwa na tukio la upandaji miti katika eneo kanisa.

Alisema ili hali ya hewa kuwa nzuri na kulifanya taifa kuwa na watu wenye utimamu wa akili ni lazima kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti mbalimbali ya matunda na kivuli.

"Ikumbukwe kuwa utunzaji wa mazingira sio mambo ambayo yanahimizwa na watawala tu bali pia ni agizo la Mungu mwenyewe kwa kuwa alipo malizia uumbaji alimwagiza Adamu kutunza bustani ya Eden.

"Watanzania wakijenga utamaduni wa kutunza mazingira yaliyo bora kwa kupanda miti na kuepukana matumizi mabaya ya ardhi ni wazi kuwa kutakuwapo na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na wakati mwingine kuzifanya jamii kuwa na afya njema na zenye furaha," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa kinamama wa kanisa hilo, (UWWT), Ester Lucosy, aliwataka wanawake wote nchini kutumia vyema fursa za maendeleo zinazotolewa na serikali.

Alisema mwaka 2025, uwe wa mabadiliko kwa kinamama kwa kuchangamkia mikopo inayotolewa na serikali kwa lengo la kuwawezesha kufanya mambo ya maendeleo.

Aidha, aliwahimiza kuwa na ujasiri wa kugombea nafasi mbalimbali za kimaamuzi katika Uchaguzi Mkuu 2025.

"Kinamama ni jeshi kubwa hivyo hakuna sababu yoyote ya kuogopa kugombea nafasi mbalimbali za kimaamuzi tunatakiwa kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi na kutoa maamuzi sahihi kwa wale tunao waongoza.

"Akigombea mtu nwenye hofu ya Mungu na kupata nafasi ni wazi kuwa atafanya kazi vizuri kwa kutekeleza sheria na taratibu za nchi kwa lengo la kulinda maslahi ya jamii na taifa," alisema.

# Magereza yaanza kutumia nishati safi kupikia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limeanza kutumia nishati safi ya kupikia katika magereza yake mbalimbali nchini ili kusaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kundokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Jeremiah Katungu, alisema hayo jana wakati wa Baraza la mwisho la Maofisa Magereza na askari wa jeshi hilo lililofanyika Msalato, Dodoma.

Alisema kuanza kutumia kwa nishati safi ya kupikia katika Magereza mbalimbali nchini ni moja ya mafanikio makubwa waliyopata jeshi hilo ndani ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mwaka 2024.

"Haya ni mafanikio makubwa sana tumeyapata katika mwaka 2024, tunaendelea kuboresha ili kuhakikisha nishati safi ya kupikia inatumika katika magereza mbalimbali hapa nchini," alisema Kamishna Jenerali.

> **"Haya ni mafanikio makubwa sana tumeyapata katika mwaka 2024, tunaendelea kuboresha ili kuhakikisha nishati safi ya kupikia inatumika katika magereza mbalimbali hapa nchini,"**

Alisema pia jeshi hilo limeanza kutumia mfumo wa Ofisi Mtandao (E-Office) kwa makao makuu kwa ajili ya kusikiliza kesi za wafungwa na mahabusu kwa njia ya mtandao.

Kamishna Jenerali Katungu alisema hiyo ni hatua kubwa kwa jeshi hilo kwa sababu inarahisisha utendaji kazi wa jeshi na inachangia kupunguza msongamano wa mahabusu katika maeneo mbalimbali nchini.

Kutokana na mafanikio hayo, Kamishna Jenerali Katungu alishukuru serikali kutokana na uwekezaji unaofanywa ndani ya jeshi hilo na kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Akielezea tathmini ya jeshi hilo kwa mwaka 2024, alisema kwenye mafanikio waliyopata ni pamoja na kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu gerezani, ikiwa ni matokeo ya ushirikiano mzuri uliopo baina ya vyombo vya haki jinai ikiwamo Mahakama, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na wadau wengine.

Alisema, mafanikio mengine ni pamoja na programu za urekebishaji magerezani kwa wafungwa zikihusisha, ushauri nasihi, kilimo, utunzaji wa mazingira, michezo na urasimishaji wa ujuzi kwa Mamlaka ya Ufundi Stadi VETA na kutoa vyeti kwa wafungwa.

Pia, alihimiza ushirikiano, umoja na upendo miongoni mwa maofisa na akitumia fursa hiyo kuwakumbusha kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura, ili wapate fursa ya kuchagua viongozi katika Uchaguzi Mkuu 2025.

Awali, akimkaribisha Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Magereza (CP) Nicodemus Tenga, alimshukuru CGP Katungu kwa kuandaa Baraza hilo ili kutoa tathmini ya utendaji wa Jeshi kwa mwaka mzima na kuwataka watendaji wote kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.



Wahitimu wa mafunzo ya ufugaji nyuki kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Katavi, Rukwa, Arusha na Tabora wakiwa pamoja juzi baada ya kuhitimu mafunzo hayo ambayo yalikuwa yanatolewa na wataalamu wa kampuni ya Kijiji cha Nyuki iliyoko Manispaa ya Singida, kupitia Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Philemon Kiemi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanafunzi wenye ulemavu wapewa msaada

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WANAFUNZI wenye ulemavu wa ngozi wanaosoma katika Shule ya Msingi Kizega, wilayani Iramba mkoani Singida, wamepewa misaada mbalimbali na Taasisi ya LBL Loyality Team yakiwamo mafuta maalum ya kuzuia mionzi ya jua.

Kiongozi wa taasisi hiyo Roda Benzi, alisema wametoa misaada hiyo ikiwamo mavazi, sare za shule, mafuta kwa watoto wenye ualbino na maandishi ya nukta nundu ili kupunguza baadhi ya changamoto zinazowakabili.

Alisema, wametoa msaada huo baada ya kuguswa na changamoto zinazokabili wanafunzi hao na kuona ni vyema wakatoa kidogo ili kiweze kuwasaidia.

Benzi, alisema kukosekana kwa baadhi ya mahitaji kwa wanafunzi husababisha kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao, LBL iliona umuhimu wa kutoa msaada ili waweze kupunguza changamoto na wanafunzi wafanye vizuri katika masomo yao.

Aidha, alitoa wito kwa jamii kuwasaidia wanafunzi wote wenye mahitaji maalum ili waweze kutimiza ndoto zao za kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Alisema LBL Royality Team itaendelea kutoa ushirikiano kwa serikali kutoa misaada kama hiyo ili iweze kuondoa au kupunguza changamoto mbalimbali za wanafunzi na watu wengine wenye mahitaji maalum katika jamii.

Mwalimu Mkuu Msaidizi Shule ya Msingi Kizega, Christopher Kirumbi alisema, licha ya serikali kuendelea kutoa mahitaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule hiyo, bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo mavazi, sare za shule, mafuta kwa watoto wenye ualibino na maandishi ya nukta nundu kwa wanafunzi wasioona.

Kirumbi alisema changamoto hizo zinakwamisha juhudi za wanafunzi hao katika masomo yao, ameiomba jamii na taasisi mbalimbali kuwasaida ili waweze kutimiza ndoto zao za kupata elimu.

Baadhi ya wanafunzi wameishukuru Taasisi ya LBL Loyality Team kwa msaada huo ambao utawasaidia kupunguza changamoto zinazowakabili.

Wameziomba taasisi na mashirika mbalimbali kutoa msaada kwa wanafunzi ambao wana mahitaji maalum ili waweze kutimiza ndoto zao.

Shule ya Msingi Kizega ina wanafunzi jumuishi ambao hawana ulemavu na wenye mahitaji maalumu ikijumuisha wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi (Albino), ulemavu wa viungo, uoni hafifu na upofu.





# Rais Mwinyi awahakikishia fidia watakaopisha miradi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewahakikishia wananchi kuwa serikali itamlipa kila mwananchi haki yake ya fidia kupisha miradi ya maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo wakati alipoweka jiwe la msingi mradi wa nyumba 370 za maakazi zilizopo Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, nyumba za fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara katika eneo la Mangapwani ikiwa ni sehemu ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani.

Dk. Mwinyi alisema kila mwananchi atalipwa kile anachotaka ikiwa malipo ya fedha au nyumba kwa kupisha ujenzi huo.

"Kila mwananchi atalipwa kwa kile anachotaka alipwe fedha na anayetaka nyumba atalipwa nyumba," alisema Dk. Mwinyi.

Rais Dk. Mwinyi aliwataka wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuchangamkia fursa za kiuchumi zitakazokuwapo kwenye miradi mikubwa ya maendeleo iliyomo mkoani humo.

Akizungumzia ujenzi wa Bandari ya Mangapwani alisema tayari mkandarasi amelipwa malipo ya awali na ameanza kazi za upimaji wa sampuli za udongo katika eneo hilo kuelekea kuanza ujenzi.

Pia, alisema kuwa serikali inakusudia kujenga uwanja mkubwa wa michezo (Football Academy) katika Mkoa wa Kaskazini Unguja utakaokuwa na viwango vya kisasa.

Rais Mwinyi ametoa pongezi kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Wakala wa Majengo (ZBA) kwa usimamizi mzuri uliofanikisha ujenzi wa nyumba hizo pamoja na mkandarasi wa ujenzi huo Kampuni ya Orkun ya Uturuki.

# Karume: Usafirishaji dawa kulevya unaathiri uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Dk. Aman Karume, amesema usafirishaji wa dawa za kulevya huathiri ukuaji wa uchumi na kusababisha kuwapo utakatishaji wa fedha haramu, rushwa na mfumuko wa bei katika nchi.

Karume aliyasema hayo huko Kidimni Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja alipozungumza katika uzinduzi wa kituo cha tiba na urekebishaji tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya.

Alisema suala hilo pia linachangia kuwapo uzalishaji mdogo wa kipato unaotokana na kupungua kwa nguvu kazi ya taifa na ukosefu wa ajira.

Aidha, kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya jamii haina budi kuchukua hatua za kuimarisha malezi bora kwa watoto na kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa tabia za vijana ili kuwalinda na makundi hatarishi na kushiriki kuwapatia elimu ya athari zitokanazo na dawa za kulevya.

Alisema vijana wanaweza kujikinga na janga hilo kwa kushiriki kwenye michezo mbalimbali, kujiepusha na imani potofu na kuacha kuiga tabia zisizokubalika katika jamii na kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii.

Aliitaka mamlaka ya udhibiti na kuzuia dawa za kulevya Zanzibar kuendelea kuwa wakali ili kuwasaka na kuwakamata wahusika wote wanaojihusisha na dawa za kulevya na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria.

Alisema utafiti mbalimbali zilizofanywa duniani zinaonesha vijana wanapotumia dawa za kulevya wakiwa na miaka 15 wanakufa wakiwa na umri uziozidi miaka 25 jambo ambalo linapoteza nguvu kazi muhimu kwa maendeleo.

Aliitaka jamii kukitumia kituo hicho kwa kuwalea watoto kupata tiba na kurekebishwa tabia na pia kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali kwa walioachana na utumiaji wa uraibu huo wa dawa za kulevya, kuacha muhali na kuendelea kuwafichua wote wanaojiusisha na biashara ya dawa hizo ili kumaliza tatizo hilo Zanzibar.

Akitoa maelezo ya kitaalamu Katibu Mkuu ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Bimaryam Juma Abdalla, alisema kituo hicho ni cha aina yake Afrika Mashariki na kina lengo la kuhakikisha kwamba kinawasaidia vijana kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya na kufunzwa, ujasiriamali ikiwamo ushonaji, ufundi magari, ufugaji, uwashi na mambo mengine ili kuwasaidia vijana walioachana na tatizo hilo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, alisema kukamilika kwa kituo hicho muhimu katika kutoa huduma za matibabu na msititizo katika mapambano na kudhibiti tatizo la dawa za kulevya kukamilika kwa kituo hicho ni sehemu muhimu katika juhudi za serikali za kuleta maendeleo ya kupambana na tatizo la athari zinazotokana na dawa za kulevya Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kudibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanal Burhan Zubeir Nassoro, alisema pamoja na mafanikio makubwa ya kupambana na suala hilo, lakini kuna changamoto kadhaa ikiwamo baadhi ya wazazi kuwasusa watoto wao licha ya kuacha uraibu huo na baadhi ya waraibu kutopenda kujiunga na kazi za ujasiriamali na stadi za kazi.

Hivi sasa Zanzibar inakisiwa kuwa na idadi ya vijana wapato 10,000 wanajihusisa na matumizi ya dawa za kulevya na kusababisha athari kubwa kwao binafsi, familia na jamii kwa jumla.



Wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wakimsikiliza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa nyumba 370 zinazojengwa eneo la Bumbwini Kidazini, Mkoa wa Kaskazini Unguja, ikiwa ni Shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Migahawa yatakiwa kuweka vyakula vinavyoimarisha afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili mstaafu Balozi Seif Ali Iddi, amesema migahawa inayotoa huduma za chakula lazima ihakikishe inaweka vyakula vitakavyoimarisha afya za wananchi ili kupunguza maradhi.

Aliyasema hayo huko Bweni nje ya mji wa Zanzibar wakati akizindua eneo la biashara na michezo na eneo hilo litakuwa linatoa huduma mbalimbali ikiwamo za chakula ambalo limejengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Balozi Seif aliwataka wafanyabiashara watakaouza vyakula katika migahawa hiyo kuhakikisha wanauza vyakula safi vinavyoimarisha afya za wananchi na sio vinavyotoa afya za wananchi.

"Wale wanatakaohuduma katika migahawa hii mpike vyakula vinavyoimarisha afya zetu ili ziendelee kuwa imara na kupunguza maradhi," alisema.

Alisema eneo hilo ambalo lina viwanja vya michezo litasaidia kuimarisha afya za wananchi kwa kufanya mazoezi ambayo ni muhimu katika kuimarisha afya za wananchi. Aidha, alisema uwapo wa eneo hilo wazazi wataondokana na hofu kwa kuwa watoto wao watakuwa wanacheza katika sehemu salama.

Aliipongeza ZSSF kwa kujitahidi kukuza uchumi na kujenga maeneo ambayo yanatoa huduma mbalimbali kwa wananchi na kuwataka kutafuta maeneo mengine kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema serikali kupitia taasisi zake zinajitahidi kuwekeza ili kuwarahisishia wananchi wake mahitaji mbalimbali ya kuondoa umaskini. Naye Waziri wa Fedha, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema licha ya kazi ya Wizara ya Fedha kuangalia sera ya fedha na uchumi, lakini ZSSF ndio inayowapa jeuri kwa sababu kazi ya mfuko huo ni kuwekeza fedha zinazokwenda kunufaisha wastaafu.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Malik Akili, alisema lengo la uzalishaji na miradi hiyo ni endelevu na alitaka taasisi zisizo za kiserikali kuwekeza katika mfumo wa huduma za jamii ili wananchi kupata maendeleo kwa sababu maendeleo yoyote ni gharama.



SEYI VIBEZ

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# BT
BURUDANI TELE





# ALI KIBA WA KIPEKEE 2025

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Ali Kiba, usiku wa kuamkia mwaka mpya amefanya kitu cha kipekee akiwa nchini Kenya, baada ya kutoa burudani licha ya mabomu ya machozi kurindima.

Haikuwa jambo rahisi kwa msanii wa muziki kuvumilia hali hiyo, lakini kwa Ali Kiba, ilikuwa kwake rahisi kwani alipanda jukwaani na kutumbuiza huku hali ya hewa ikiwa imechafuka kwa mabomu.

Katika shoo hiyo iliyofahamika kama Raha Festival iliyofanyika jijini Nairobi katika kuukaribisha mwaka mpya, mashabiki na wapenzi wa muziki walikabiliana na polisi kufuatia kujitokeza kwa kundi la watu waliotoa sauti ya kumtaka Rais Ruto kuondoka madarakani.

Wachambuzi wa muziki, wanasema alichokifanya Ali Kiba, ni jambo la kupongezwa kwa sababu amewatendea haki msshabiki wake ambao walikwenda hapo kupata burudani.

John Kalimbo, amesema ujasiri alionyesha Ali Kiba kuimba huku mabomu ya machozi yakitupwa na polisi, ni wa kipekee kwani angekuwa msanii mwingine angeondoka jukwaani na kutorudi tena.

"Ali Kiba amewafundisha wasanii wenzake namna ya kuheshimu kazi, hakujali mabomu ya machozi, yeye aliwathamini mashabiki wake waliomfanya aende Kenya. Tumpongeze kwa ujasiri wake wa kipekee,' amesema kalimbo.

Kalimbo amewashauri wasanii wanaopata kazi za nje ya nchi, kuiga mfano wa Ali Kiba, kwani kuondoka jukwaani kwa hali yoyote ni kuwakosea wapenzi na mashabiki wa muziki ambao wamelipa pesa kwa ajili ya kupata burudani.

BASI SAWA

## Akothee hashawishiki




MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Akothee amesema hawezi kusogelea sigara na bangi kwa sababu harufu yake inakuwa vigumu kuizoea.

Akothee amesema kuna wakati rafiki yake alijaribu kumshawishi kutumia bangi kwa madai inaongeza akili. Lakini alikataa na kuhoji mantiki ya rafiki yake huyo.

“Kuna mtu anajaribu kunishawishi kuwa bangi haiathiri haiba ya watu au akili, lakini inawafanya wawe werevu zaidi. Mimi binafsi naona harufu ya sigara haivumiliki,” amesema kupitai ukurasa wa Instagram.

## Shakib aonyesha upendo kwa watoto wa Zari



MTOTO wa pili wa nyota wa mitandao kutoka Uganda, Zari Hassan, anayeitwa Raphael Ssemwanga, amesherehekea siku yake ya kuzaliwa kwa ujumbe wa kushangaza kutoka baba yake wa kambo Shakib Cham.

Shakib akionekana kuwa na upendo kwa mtoto huyo aliandika ujumbe ambao unaonyesha jinsi anavyompenda na kumjali kama mtoto wake.

“Heri ya siku ya kuzaliwa @raph, natumai kuwa leo ni mwanzo wa mwaka mzuri kwako,” aliandika Shakib na kuweka picha ya Raphael.



# MBOSSO HUYU BINTI UTAMPATA

MWANAMUZIKI maarufu wa kizazi kipya, Mbosso, ametangaza kumsaka msanii chipukizi Lydia Bleck kwa ajili ya kufanya naye kazi.

Lydia ambaye alikuwa mshiriki wa BSS na kisha kutolewa, amekuwa gumzo baada ya kufanya vizuri katika nyimbo anazozirudia za wasanii wakongwe.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Mbosso aliweka picha ya Lydia na kuandika kwamba anamsaka binti huyo kutokana na kuonyesha uwezo mkubwa wa uimbaji.





# Madee bora unakumbuka wema

MWANAMUZIKI Mkongwe wa Bongo Fleva, Madee, amesema Mungu alikuwa na kusudi lake kumkutanisha na Babu Tale, kwani amepata manufaa mengi kupitia yeye.

Akizungumza hivi karibuni, Madee amesema yeye na Babu Tale hawakukutana tu mtaani, bali urafiki wao umekuwa kama ndugu na kwake anaona ufahari.

“Sisi hatujakutana kutana tu kama kina Roma wanavyokutana baada ya wiki mnachambana. Sisi tulikutanishwa na Mungu na alikuwa na kusudio lake na limetimia,” ameandika Madee kupitia ukurasa wake wa Instagram.

FILAMU

# Maigizo: Siri ndani ya siri

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA hii imeficha siri nyingi sana na kama siku itaamua iziweke bayana, basi watu wanaweza kukimbiana.

Mungu alipoweka kitu siri ilikuwa na maana yake, na kama binadamu angekuwa anafanya yote yanakuwa peupe, sijui angebaki nani duniani.

Ukiifutilia filamu hii ‘Maigizo’ utakutana na vitu ambavyo vitakufikirisha sana. Lakini ndiyo dunia ilivyo kwani huwa vinatokea kwenye jamii yetu.

Kufinya anaishi na mkewe Ashura. Kufinya ana mdogo wake Madebe Lidai ambaye kwenye filamu ametumia jina la Mbulu.

Mbulu ni mlevi, mwizi na akakaa na kaka yake hapo hapo, huku akilipiwa kodi. Kila siku ni wizi na Kufinya na mkewe kazi yake kubwa ni kwenda kumtoa kwenye vituo vya polisi na kulipa madeni ya watu.

Ashura anamwambia mumewe amechoka kuishi na Mbulu, hivyo kama hatomtoa hapo, basi yeye atarejea kwao ili amuache na mdogo wake.

Kufinya hataki kuliona hili la mkewe kuondoka, hivyo kila siku anagombana na mdogo wake.

Mbulu naye anamtuhumu kaka yake kuwa anamsikiliza sana mkewe na ametawaliwa kiasi cha kumuona yeye kama hana maana.

Hali hiyo inamchanganya Kufinya, kwani anapata lawama pande zote mbili za mkewe na mdogo wake.

Kwenye nyumba hiyo hiyo anaishi Mwanjala na mkewe. Mkewe Sauda amekuwa na tabia ya kuaga kwenda sehemu mbalimbali na mumewe anamkubalia. Kuna siku akaaga anakwenda kwa dada yake, lakini baada ya muda dada mtu akafika pale. Hiyo ikaanza kumtia wasiwasi.

Kufinya hali ya mdogo wake ilivyodizi kuwa mbaya kwa wizi, akaamua kumfukuza nyumbani.

Mbulu akaanza kuishi kwa washkaji na kutangatanga, kwani hata kula sasa ikawa hali nyumbani.

Siku isiyo na jina alimfuata Mwanjala na kumwambia anataka kumpa zawadi. Lakini akamwambia hanayo pale amfuate. Akampeleka hadi sehemu wakagonga mlango. Ulipofunguka, Mwanjala hakuamini macho yake.

Ni kwamba mkewe alikuwa yupo na Kufinya. Kumbe ni hawara yake kitambo. Na Mbulu amewachoma kwa ajili ya kulipa kisasi cha kutimuliwa na kaka yake nyumbani. Kumbe alikuwa anajua siri ile.

Sauda anawekwa kikao cha kuulizwa kisa cha kutembea na mume wa mpangaji wenzake.

Akasema wameishi na Mwanjala kwa muda mrefu bila kupata mtoto kitu ambacho kinamsumbua kwa mawifi zake, hivyo akaamua kutembea na Kufinya ili apate mtoto kwa sababu mkewe Ashura ni mjamzito.

Mama mmoja jirani akaja na kukuta zogo hilo, baada ya kuhadithiwa, akatoa siri nyingine kuwa huenda familia ya Kufinya ina tabia hiyo, kwani awali kumfuma Mbulu akifanya mambo yasiyofaa na shemeji yake Ashura.

Kufinywa kusikia hivyo akaanguka na kuzimia. Kumbe Mbulu alikuwa anafanya maigizo ya kugombana shemeji yake Ashura kuonekana hawaelewani, ili kumpoteza maboya Kufinya kumbe ni wapenzi.

Hata ujauzito wa Ashura ambao Sauda alidhani ni wa Kufinya na kutembea naye kumbe ni wa Mbulu.

# WASANII WALIOMALIZA 2024 KIBABE

**Na Adam Fungamwango**

MWAKA 2025 bado mbichi kabisa, ukiwa na siku nne tu. Wasanii mbalimbali wa muziki wa bongo fleva saa hizi wanapigana vikumbo kuingia na kutoka studio kwa ajili ya kutoa ngoma mpya.

Wiki ijayo tutapata muda wa kuwafahamu wasanii walitoa ngoma mpya mwanzoni tu wa mwaka huu.

Leo tuwaangalia wasanii ambao walitoa ngoma zao mwishoni mwa mwaka 2024. Kuna ngoma ambazo zilitolewa mwezi Desemba mwaka jana ambazo zimeingia kwenye kumbukumbu ya kufunga mwaka. Hawa ndiyo wasanii waliofyatua nyimbo zilizofungia mwaka na hizi ndizo ngoma zao.

**Marioo feat Harmonize - Wangu**

Siku tatu tu baada ya Desemba mwaka jana, msanii Marioo alifyatua ngoma aliyoiita ‘Wangu’, akimshirikisha gwiji, Harmonize.

Ni moja kati ya ngoma kali zilizofunga mwaka, na hadi jana ilikuwa kwenye nafasi ya saba kwa ‘kutrendi’, kwenye mitandao ya kijamii.

**Dully Sykes & Alikiba - Zali**

Mmoja wa wakongwe na waanzilishi wa muziki wa kizazi kipya nchini, Dully Sykes, Desemba 6 mwaka jana, alipua ngoma moja kali akaipa kina la ‘Zali.’ Akamshirikisha mkongwe mwenzake, Ali Kiba.

Hadi kufikia jana, ngoma hii ilikuwa nafasi ya tatu kutazamwa na watu wengi ni mitandao ya kijamii.

**Maua Sama feat Alikiba - Itakuwaje**

Mwanadada Maua Sama, naye alimaliza mwaka 2024 vizuri tu kwa ngoma yake iitwayo, ‘Itakuwaje.’

Alitoka rasmi Desemba 15 mwaka jana, akaamua kumshirikia Ali Kiba.

**Rayvanny feat Phina - Ataniua**

Kesho yake, Desemba 16, msanii Rayvanny akimshirikisha mwanadada, Phina, walimaliza mwaka kwa kishindo kwa ngoma ya aina yake, ‘Ataniua.’

Ni ngoma inayomzungumzia mwanadada anayeteseka kwa mwanaume asiyependeka. Ngoma ina maneno yafuatayo.

“Nina mkosi gani, nyumbani imekuwa vitani, hatuelewani, hivi nimekosa kubwa gani, sina thamani, aah nateseka jamani, najiona mjinga wa mapenzi, ananitenda ila bado namng’ang’ania, anajua nampenda ndiyo maana anafanya naumia. Nikimpigia simu anakata namsumbua, nikilalamika nayazua, mwepesi kuchukua hatua, juzi kanipiga nusu ya kuniua, hospitali zote wananijua, nishashunwa alipopasua, majirani wote wanajua uvimbe ikizidi mwenyewe najichua.” Ni hatari kwa kweli.

Binti alikuwa amekwenda kushtaki kwa kaka yake, naye anamshauri kwa maneno haya.

“Kama kakuchoka rudi nyumbani, una ng’ang’ania mateso ya kazi gani? Hawezekani kila siku kama mko vitani, ukilia dada nakosa amani.”

**Phina ft Harmonize - Bye Bye**




Phina, baada ya kushirikishwa na Rayvanny, na yeye akaja na ngoma yake akiita, ‘Bye Bye.’

Hadi jana ilikuwa kwenye nafasi ya tisa kwa ‘kumtrendi’.

Phina akaamua kumshirikisha Harmonize katika ngoma hiyo.



# Huyu ndio Burna Boy

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Burna Boy, amejitokeza hadharani na kujitetea kuwa shabiki aliyemvamia jukwaani alivunja sheria zake.

Msanii huyo ameibua mjadala baada ya video kuonyesha akiondoka jukwaani wakati wa onyesho lake kwenye tamasha la Greater Lagos.

Hata hivyo, mwenyewe amesema alipewa dakika kumi pekee ya kutumbuiza, lakini aliimba kwa saa moja.

"Ilikuwa onyesho la bure. Nilipaswa kufanya dakika 10 na nilifanya karibu saa moja. Kila mtu anajua sheria yangu kuhusu kupanda jukwaani na kunishtua ninapotumbuiza. Usiruke kwenye jukwaa langu hivyo," amesema.



## Nini kilimponza Seyi Vibez?

RAPA mkali kutoka Nigeria, Seyi Vibez, amekuwa kimya baada ya video iliyosambaa mitandaoni ikimwonyesha msanii huyo akitolewa kwa nguvu katika tamasha la muziki jijini Lagos.

Msanii huyo ambaye hivi karibuni aliondoka katika lebo ya Dapper, hajasema chochote kuhusu sakata hilo ambalo limesababisha mashabiki wake kuwa na hasira.

Katika video hiyo, msanii huyo ameonekana akibebwa kwa nguvu na walinzi hadi nje ya eneo lililofanyika tamasha hilo.

## Uche ataka mke wa pili kijanja

MWIGIZAJI mwenye utata kutoka Nollywod, Uche Maduagwu, ametabiri kuwa mwaka 2025 msanii mwenzake Yul Edochie atakuwa na mwanamke mwingine.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Maduagwu, alifichua utabiri huo kuwa alifunuliwa na mamlaka ya juu kwamba Yul Edochie atapata mtoto mwingine na mwanamke huyo.

Uche Maduagwu alimuomba mke wake amruhusu kuwa na mwanamke mwingine, kwa sababu Yul tayari anatarajia kupata mtoto na mwanamke mwingine.





## Portable hataki kupoa

MWANAMUZIKI ambaye anapendwa na vijana wa mitaani, Portable amemwita mchungaji Adeboye kuwa ni mwongo wa kiwango cha juu.

Mchungaji huyo alitoa utabiri wake wa mwaka mpya 2025, akieleza taifa la Nigeria litashuhudia vurugu kutokana na watu kushindwa kuvumilia kwa baadhi ya mambo.

Hata hivyo, Portable, amesema mchungaji huyo anaongopa na kwamba hata mahubiri yake anayatilia shaka kutokana na kwenda kinyume na Biblia.

## BlasketMouth afichua penzi lenye sumu

MCHEKESHAJI wa Nigeria, Bright Okpocha maarufu BasketMouth ametoa siri jinsi alivyojinasua katika mapenzi aliyoyaita kama sumu.

Alisema kwamba akiwa katika uhusiano huo alibaini anazidi kunyonywa na hapo ndipo alipoamua kurudi nyuma na kuachana naye.

Basketmouth amefichua kuwa kama angeendelea katika uhusiano huo hali yake ingebadilika kutoka kuwa mnene hadi mwembamba wa kutisha.





# Babu kuweka ‘mashushu’ kuwachunguza wakuu wa shule

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema atawatuma kwa siri watu aliowaita ‘mashushu’ kuwachunguza wakuu wa shule za sekondari na walimu wakuu wa msingi, ambao watakaokanyaga mwongozo wa kitaifa wa ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalum ya elimu.

Amesema anataka kujiridhisha kuhusu jambo hilo, akisisitiza hataki mzaha katika mapokezi ya wanafunzi wenye ulemavu, kwa kuwa serikali imeweka miundombinu rafiki kwa watoto hao.

Alidokeza kuhusu mpango wake wa kusimama na wenye ulemavu kupata haki ya kielimu, baada ya kukagua miradi ya ujenzi na ukarabati wa shule sita zilizoko Wilaya za Siha, Hai na Moshi, juzi.

“Tutafanya utaratibu na TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), kuona namna ya kupata walimu watakaosaidia hasa katika zile shule mpya zitakazopokea wenye mahitaji maalum. Kilimanjaro, tumejipanga kuhakikisha watoto wote wanapata elimu bora. “Nitatuma watu wangu kimya kimya wanipigie picha na kama hamjamaliza tutaelewana vibaya.”

**“Tutafanya utaratibu na TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), kuona namna ya kupata walimu watakaosaidia hasa katika zile shule mpya zitakazopokea wenye mahitaji maalum.**

Mwongozo wa kitaifa wa ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu wa mwaka 2023 na Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (MKEJ), unaelekeza kuwa utoaji wa elimu kwa wote bila ubaguzi, utachangia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa Taifa la Tanzania, ambayo ni ya haki, usawa na ujumuishi.

Aidha, aliwataka wazazi/walezi wenye changamoto ya ukuaji wa kiakili na kimwili, kutowaficha ndani watoto hao, badala yake wapelekwe shule ili wapate elimu.

Akizungumzia tabia iliyojengeka katika jamii ya kuficha watoto wenye mahitaji maalum, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la TUSONGE CDO linalofanya kazi na jamii ya wenye ulemavu, Aginatha Rutazaa alisema:

“Jamii imekuwa ikiwaficha ndani wasionekane, lakini kumbe ndani wana utajiri mkubwa, wakitoka nje kufundishwa na kushirikiana na wengine wataleta furaha, ambayo Tanzania na ulimwengu unaitafuta katika fedha na mambo mengine.”



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (wa tatu kushoto), akifurahia jambo na Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa pili kushoto), walipotembelea maendeleo ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari ambayo ni ya tatu katika awamu hii, Kata ya Kaloleni pamoja na madarasa matatu mapya ya Shule ya Msingi Juhudi hivi karibuni. Wengine ni viongozi kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja baadhi ya madiwani na menejimenti ya Manispaa ya Moshi. **PICHA: JAMES LANKA**

## Shule zote kuwekeza miundombinu muhimu

**Na Godfrey Mushi,** MBULU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali itahakikisha shule zote za umma zinawekeza katika miundombinu, ikiwamo umeme na elimu ili kuziepusha shule hizo kuteseka kwenye matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Prof. Mkumbo alidokeza hayo jana, alipokuwa akizungumza katika Kata ya Silaloda, Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, wakati akiweka jiwe la msingi na kuzindua mradi wa umeme wa Silaloda.

Mradi huo umegharimu serikali Sh. milioni 146.18, fedha ambazo zilipokewa mwaka wa fedha 2023/2024.

Waziri Mkumbo, alisema mradi huo ni sehemu ya juhudi za serikali kuimarisha miundombinu, ikiwamo umeme na elimu, huku akibainisha kuwa umeme huo tayari umesambazwa kwenye shule mbalimbali, ikiwamo Sekondari ya Silaloda.

Awali, Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Wilaya ya Mbulu, Bura Nyoka, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Februari na kukamilika Juni mwaka jana, ukihusisha usambazaji wa umeme katika Shule na Zahanati ya Silaloda.

Mbali na mradi huo wa umeme, Prof. Mkumbo, alizindua mradi wa ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana kwa ajili ya kidato cha tano na sita, madarasa sita na matundu tisa ya vyoo katika Shule ya Sekondari Kainam, wilayani Mbulu, wenye thamani ya Sh. milioni 428.9.

Alisema lengo la mradi huo ni kuongeza miundombinu kwa ajili ya kidato cha tano na cha sita, na kutoa nafasi kwa wanafunzi wengi kujiunga na shule hiyo. Alitoa wito kwa wananchi wa wilaya hiyo kutumia fursa ya uwekezaji mkubwa wa serikali kupeleka watoto kupata elimu na kuondoa desturi ya kuozesha mabinti wakiwa na umri mdogo.

Mkuu wa shule hiyo, Emanuel Nikodemus, alisema kuwa mradi huo ulileta manufaa makubwa kwa wanafunzi na wadau wa elimu, kwa kuwa idadi ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita imeongezeka kutoka 44 hadi 612.

# Dawa kuwaangamiza ‘Kantangaze’ yagundulika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKULIMA wa nyanya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wanaopoteza jasho lao shambani kutokana na kusumbuliwa na wadudu waharibifu wa mazao ‘Kantangaze’ (Tuta Absulute), sasa wamepata ahueni baada ya watafiti kugundua namna mpya ya kuwaangamiza kwa kutumia homoni maalum.

Mtaalamu wa Kilimo Biashara wa Shirika la World Vegetable Center, Judith Assenga, akizungumza jana na wakulima wa nyanya katika shamba mafunzo Kijiji cha Masaera, Kata ya Makuyuni, alisema mdudu huyo amekuwa tishio kwa zao hilo kutokana na uwezo wake wa kushambulia na kuhatarisha uhakika wa mavuno kwa asilimia 80 mpaka 100.

Mradi huo wa Agroveg, unaotekelezwa na Shirika la World Vegetable Center katika Wilaya ya Moshi, umeanza kuleta tija kwa kupunguza uzalishaji wa nyanya kwa kutumia viuatilifu vya sumu. Mradi huo wa miaka mitatu, unafadhiliwa na Biovision kupitia Taasisi ya ICIPE.

“Kwenye zao la nyanya, tunajitahidi sana kupunguza matumizi ya dawa. Tunayo teknolojia ya kwanza, ambayo tunaita homoni maalum, ambazo zinavuta wale wadudu wa kantangaze.

“Tunatumia kilimo cha mzunguko, ambacho ukilima nyanya, mwisho wa siku ukivuna zile nyanya, hupaswi kurudia tena kulima nyanya na hiyo ndio mwarobaini wa kumwangamiza kantangaze.

“Nawashauri wakulima wajitahidi sana kuchukua hii teknolojia ya kuvuta na kusukuma wadudu (Push Pull Technology), kwa kutumia mazao mchanganyiko, kwa kuwa hii teknolojia ni nzuri kwao, kwa sababu inawapunguzia matumizi makubwa ya gharama shambani.

...Faida ya mkulima inapunguzwa sana na matumizi makubwa ya dawa shambani. Pili, nawashauri watuimie hii teknolojia kwa sababu ni teknolojia ambayo itamlinda yeye na afya ya mlaji.”

Mtaalamu wa Afya ya Mimea wa World Vegetable Center, Dk. Simon Boniface, alisema kuhusu afya ya udongo, kemikali zinaharibu sio tu afya ya viumbe vinavyokuwa juu ya ardhi, bali vile vinavyokuwa ndani ya ardhi.

Alisema kuna minyoo, ambao ni muhimu sana kwenye afya ya ardhi, lakini kuna vimelea kama fangasi na bakteria, ambao wanachakata yale masalia ya mimea ndani ya ardhi kuweza kutoa virutubisho ambavyo vinaweza vikatumika na mmea.

“Kwa mfano unaweka samadi kwenye shamba, vimelea ndivyo vinavyoichakata kwa kuivunjavunja ili yale madini ambayo mmea unaweza ukachukua. Lakini minyoo iliyopo inatengeza njia na mashimbo ambayo ni muhimu sana kwenye rutuba ya udongo, ambako kutakuwa na hewa na maji yakapita vizuri.

...Kama fangasi au bakteria, ambao wanawashambulia kantangaze, na wenyewe kwa pamoja tukichanganya kwa kutumia teknolojia tunayoita kitaalam Integrated Pastes Management (IPM), kwa Kiswahili tunawezasema kwa kutumia njia shirikishi na jumuishi kwa pamoja. Njia tofauti tunazichanganya kwa pamoja ili kupambana na tatizo lililopo.”

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mikasa ya mapenzi tangu enzi na enzi

## -'Photo album', gauni, picha vyavunja ndoa

**Na Adam Fungamwango**

WAMENIAMBIA mambo yako mama eee, wamenieleza matatizo ya mume wako eee, ya kisa cha wewe sheri Zinduna, kufika kupewa talaka." Ni mwanzo wa wimbo uliotungwa na gwiji la muziki Tanzania, Zahir Ally Zorro. Ikumbukwe kuwa mwanamuziki huyu ndiye baba wa mwanamuziki Banana Zorro.

Ni wimbo ambao una kisa kimoja cha ajabu na kusikitisha sana. Nimeamua kuja na mada hii leo ili tuangalia jinsi wanamuziki wa zamani walivyokuwa na uwezo wa kuchua visa vya kweli kabisa na kuviweka kwenye muziki, vikafundisha, kuelimisha, kufurahisha na kufikirisha watu.

Hiki ni kisa cha ukweli kabisa kilichotokea kwenye miaka ya 1980.

Ni kisa cha picha iliyopigwa zamani katikati ya jiji la Dar es Salaam, lakini ikaenda kuvunja ndoa miaka mingi baadaye jijini Mwanza. Hebu tuendelee na mashairi ya wimbo huu.

*"Photo albamu inaleta maneno, katikati ya jiji la Mwanza, kisa ni picha iliopigwa zamani, katikati ya Dar es Salaam. Sheri Zinduna nakupa pole Zinduna. Matatizo yanayokukuta. Mkasa nyumbani kwako, ndoa imevunjika, kisa ni picha ya zamani ooo. Afadhali kama mimi ningewahi kufika Mwanza, lakini tangu mimi nimezaliwa, sijafika Mwanza ooo. Vitongoji vya Namanyoro, Kirumba na Mtaa wa Sukuma, nimeelezwa na wenyeji ooo."*

Hapa ndipo wimbo huo ulipokamilika.

Maudhui ya wimbo huu, ni kwamba huyu dada Zinduna aliolewa na jamaa jijini Mwanza. Lakini kabla ya kuolewa alikuwa na mpenzi wake. Waliwahi kupiga picha katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Mwanadada huyo inaonekana alihifadhi picha hiyo sehemu ambayo anaijua yeye hata baada ya kuachana na mpenzi wake huyo na kupata mchumba ambaye alikuja kumuoa, akawa mumewe.

Baada ya kuolewa, makazi ya Zinduna na mumewe yakahamia jijini Mwanza kutoka Dar es Salaam.

Kilichotokea baada ya miaka michache, mume wa Zinduna aliifuma picha ya mkewe aliyopiga na mpenzi wake katikati ya jiji la Dar es Salaam. Sijui ilikuwaje, lakini aliifuma picha hiyo iliyofichwa vizuri kwenye 'photo albamu'.

Mume alichanganyikiwa, na kwa bahati mbaya sana ni kwamba gauni alilovaa Zinduna lilifanana sana na lile alilomnunulia siku chache zilizopita.

Mume akiangalia anaona ni kama picha ya zamani ambayo haikupigwa Mwanza, lakini hayo yote yanamezwa na gauni hilo alilomnunulia hivi karibuni. Akawa anajiuliza kama ni picha ya zamani, mbona gauni hili ndiyo hilo alilomnunulia majuzi. Kwa hiyo akadhani kabisa kuwa picha hiyo haikupigwa siku nyingi. Kwa hiyo akaona kabisa kuwa kumbe mkewe anamsaliti.

Pamoja na Zinduna kujitetea kwa anavyojua kuwa picha hiyo ni ya mpenzi wake wa zamani, miaka zaidi ya kumi iliyopita kabla hata ya kukutana na yeye, tena ilipigwa Dar es Salaam, mume hakukubali. Kilichofuata ni talaka. Zinduna alilia na kusononeka. Akarejea kwao Dar es Salaam.

Mpenzi wa zamani ambaye alipiga naye hiyo picha akasikia habari hizo. Alisikitika sana na hakujua afanye nini ili amsaidie, kwani naye alikuwa ameshaoa. Basi akabaki na yeye analalamika na kumpa pole mpenzi wake wa zamani Zinduna.

Anayesikika anaimba kwenye wimbo huo kwa jinsi ulivyopangiliwa, ndiye mpenzi wa zamani wa Zinduna, anamwambia wameniambia mambo yake na matizo yake na kisa cha mpenzi wake wa zamani Zinduna kufika kupewa talaka, kisa ni 'photo albamu' iliyokuwa na picha waliopiga zamani katikati ya Dar es Salaam, ikaleta maneno jijini Mwanza.

"Alipaswa baba watoto ajue, sijawahi kufika Mwanza, toka mimi nizaliwa, sijafika Mwanza." Jamaa anamfariji mpenzi wake wa zamani, kuwa mumewe alipaswa ajue kuwa yeye hajawahi kufika Mwanza tangu azaliwe, hivyo hiyo picha siyo ya hivi karibuni, bali ya zamani kabla hajaolewa. Kama angewahi kufika Mwanza, basi angeweza kuwa na wasiwasi kuwa amepiga picha na mkewe, lakini vitongoji vyote anavisikia kwa watu.

Wimbo huu uikumbusha jamii kuwa kuna wakati watu wanafanya maamuzi makali na magumu kwa vitu ambavyo hawajavifanyia utafiti wa kutosha, au kufanya upepelezi, bali ni hasira na mihemko.

Ni kwamba inafaa kwanza kabla ya kuamua jambo lolote hasa lenye mustakabali wa maisha yetu ni lazima tujiridhishe kwanza. Zinduna amepewa talaka kwa kosa ambalo hajalifanya. Na mumewe kama alikuja kujua hilo baadaye anaweza kumshawishi mkewe warudiane? Na kama akikataa kuna kosa?

**Meseji namba: 0716 350534**





Zahir Ally Zorro

HABARI KIMATAIFA

# KIZAAZAA NJE YA IKULU

## -Rais Korea Kusini chupuchupu



Rais Yoon Suk Yeol

**SEOUL,** KOREA KUSINI

KIZAAZAA kimeibuka Korea Kusini wakati kikosi cha upelelezi nchini humo kilipojaribu kumkamata Rais aliyesimamishwa Yoon Suk Yeol, ambaye amejificha katika jengo la Ikulu ya nchi hiyo.

Hata hivyo, mabishano makali yalidumu kwa muda wa saa sita kati ya wachunguzi, polisi na wanajeshi wanaomlinda ilifanya zoezi la kumkamata kiongozi huyo kusitishwa.

"Tumebaini kwamba kukamatwa hakuwezekani," ilisema ofisi ya upelelezi wa ufisadi (CIO), ambayo imekuwa ikichunguza tamko la amri ya sheria ya kijeshi ya muda mfupi iliyotolewa na Yoon mwezi uliopita.

"Hatua zinazofuata zitaamuliwa baada ya kutathminiwa upya," CIO ilisema katika taarifa yake, na kuongeza kuwa kukataa kutekeleza mchakato wa kisheria kwa Yoon ni jambo la kusikitisha.

Wafuasi wa Yoon, ambao walipiga kambi mbele ya majengo ya Ikulu yaliyoko mji mkuu wa Seoul, kwa siku kadhaa kupinga kukamatwa kwake.

Wakati taarifa ya kusitishwa kwa zoezi hilo likitolewa, wafuasi hao walishangilia kwa kuimba nyimbo na kucheza dansi.

"Tumeshinda!" waliimba kwa nguvu wafuasi hao.

CIO ilisema kuwa wamechukua hatua hiyo kutokana na wasiwasi wa usalama kwa timu ya wachunguzi katika uwanja wa Ikulu.

Katika amri iliyotolewa na mahakama, wachunguzi hao wana muda hadi Januari 6 kumkamata Yoon kabla ya hati hiyo kuisha.

Hata hivyo, wanaweza kuomba hati mpya ya kumweka kizuizini tena.

**HALI ILIVYOKUWA**

Tangu asubuhi asubuhi ya jana, makumi ya gari za polisi yalijipanga barabarani nje ya makazi ya Rais Yoon katikati mwa Seoul.

Ofisi ya Juu ya upelelezi wa uhalifu wa viongozi wa Umma inayopeleleza makosa ya ufisadi ilitangaza kwamba itaanza kutekeleza agizo la kukamatwa kwa Rais Yoon Seok-yeol jana saa 2:07 asubuhi, lakini jaribio hilo lilionekana kuwa gumu na lenye hekaheka.

Inaarifiwa kuwa timu ya wachunguzi na polisi wapatao 80 kutoka Shirika la Uchunguzi wa Ufisadi walioingia kwenye lango kuu la makazi ya Yongsan kwa nia ya kwenda kumkamata.

Hata hivyo, wakati wanaingia walikumbana na mtafaruku kutoka kwa walinzi na wanajeshi ambao walizuia kushindwa kuingia ndani ya jengo hilo.

Wachunguzi wa taasisi ya uchunguzi wa rushwa yalianza safari kutoka hilo la Serikali la Gwacheon mwendo wa saa 12:14 asubuhi na kufika karibu na makazi ya Rais huko Hannam-dong mwendo wa saa 1:20 asubuhi.

Kwasababu lango kuu lilikuwa limefungwa na magari, wachunguzi wapatao 80 kutoka Ttasisi ya uchunguzi wa rushwa na polisi waliingia ndani ya nyumba hiyo kwa miguu.

Majibizano yaliibuka kati yao na wafanyakazi wa usalama, lakini waliingia hadi lango kuu bila kupata upinzani mkali.

Lakini walishindwa kuingia ndani ya jengo hilo kupitia lango kuu kutokana na walinzi wa rais kuwazuia.


**MTU WA BAHATI**

Mnamo Januari 2, polisi walikadiria kuwa watu 10,000 walikusanyika karibu na makazi ya rais huko Hannam-dong, Yongsan-gu mjini Seoul, kumlinda Yoon asikamatwe

Ofisi ya Upelelezi wa ufisadi ilipokea hati ya kukamatwa na hati ya upekuzi kutoka mahakama kuu Desemba 3, baada ya Rais Yoon kushindwa kukataa kutii agizo la kujisalimisha mara tatu.

Ingawa hakukuwa madhara katika eneo la tukio, baadhi ya wafuasi walipambana na polisi na waandamanaji kushinikiza kiongozi huyo kujisalimisha.

**BBC**



Gari lililokuwa limebeba wachunguzi wa shirika la uchunguzi wa ufisadi liliwasili likiwa limezuiwa nje ya makazi ya Rais Yoon Suk Yeol, majira ya saa 1:20 asubuhi ya jana.

# Israel yaua Wapalestina 50 Gaza

**GAZA,** PALESTINA

ISRAEL imefanya mashambulizi ya anga katika Ukanda wa Gaza na kusababisha vifo vya watu 50, huku juhudi za kusaka makubaliano ya usitishwaji mapigano zikiendelea.

Mashambulizi hayo yalianza juzi na kuendelea hadi Ijumaa, yaliyalenga maeneo ya kati ya Deir al Balah na kusini mwa Gaza katika mji wa Khan Younis ambako polisi watano waliuawa.

Msemaji wa serikali ya Israel, David Mencer alisema shambulio hilo lilikuwa likimlenga ofisa mwandamizi wa Hamas , na kulitupia lawama kundi hilo kwa vifo vya raia.

"Shambulio la anga lililoongozwa na idara ya ujasusi usiku kucha, lilimlenga Hossam Shahwan, mkuu wa kikosi cha usalama wa ndani cha Hamas kusini mwa Gaza. Tungempata wapi? Si mahali pengine, bali alikuwa kajificha katika eneo la kiraia huko Khan Younis, ambako raia wa Gaza wamejihifadhi ili kujikinga na vita hivi," alisema Mencer.

Kambi ya al-Mawasi inayowahifadhi Wapalestina kwenye mahema ambayo mara kadhaa Israel imeitaja kuwa eneo salama la kibinadamu.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ilisema imeidhinisha ujumbe kutoka idara ya upelelezi (Mossad) na ile ya usalama wa taifa (Shinbet) ili kuendelea na mazungumzo nchini Qatar kuhusu kupata makubaliano ya kumaliza vita.

Wapatanishi kutoka Marekani, Qatar na Misri wametumia muda wa karibu mwaka mmoja kujaribu kufikiwa kwa mpango wa usitishaji mapigano na kuachiliwa kwa mateka, lakini mara kadhaa juhudi zao zimekuwa zikiambulia patupu.

**DW**

# Zimbabwe yapongezwa

**HARARE,** ZIMBABWE

UMOJA wa Mataifa umeipongeza Zimbabwe kwa kuondoa hukumu ya kifo, na kuzitaka nchi nyingine kuchukua hatua kama hiyo, au kusitisha kwa muda adhabu ya kifo.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, Jumanne alisaini sheria ya kuondoa adhabu ya kifo, hatua ambayo itabatilisha adhabu hiyo kwa wafungwa 60 ambao walihukumiwa kunyongwa.

Kamishna Mkuu wa Haki za Binaadamu wa Umoja wa Mataifa,Volker Turk, alisema anaipongeza hatua ya Rais Mnangagwa kuondoa rasmi adhabu ya kifo.

Sheria ya Kukomesha Adhabu ya Kifo nchini Zimbabwe inaeleza kuwa sasa mahakama haziwezi tena kutoa hukumu ya kifo, na hukumu zozote za kifo zilizopo lazima zibadilishwe na kuwa kifungo gerezani.

Hata hivyo, kipengele kimoja kinasema hatua ya kukomeshwa kwa hukumu ya kifo inaweza kuondolewa wakati wa hali ya hatari.

**DW**

# 'Special hire' sasa kuunganishwa VTS

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewataka wamiliki wa mabasi maalum ya kukodi, maarufu kama 'Special Hire' kuyaunganisha katika Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS).

Kadhalika, imetaka madereva ambao bado hawasajiliwa kwenye Kitufe cha Utambuzi wa dereva maarufu i-button, kusajiliwa na kuunganishwa na mfumo huo kabla ya Januari 12, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, Salum Pazzy, ni takwa la kisheria mabasi hayo kusajiliwa katika mfumo huo.

"Kwa mujibu wa kanuni ya 20(b) ya kanuni za Mamlaka ya Usafiri Ardhini za magari ya kukodi za mwaka 2020, mabasi maalum ya kukodi (Special Hire), yanapaswa kuunganishwa na VTS.

"Mfumo huo huwezesha mamlaka kumtambua dereva anayeendesha gari husika endapo atasajiliwa na kutumia kitufe hicho cha utambuzi wa dereva," alisema Pazzy.

Alisema, kanuni ya 9(2), ya kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za uthibitishaji madereva na usajili wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara, mamlaka ina jukumu la kuainisha magari yanayopaswa kutumia kitufe cha utambuzi wa dereva na mabasi maalum ya kukodi ni miongoni mwa magari yaliyoainishwa."

Pia, alisema kanuni ya 9(3) inamtaka dereva aliyepewa kitufe cha utambuzi kuhakikisha kitufe hicho kiko salama na hatakiwi kumpatia mtu mwingine.

Kwa mujibu wa Pazzy, mamlaka hiyo inawakumbusha madereva na wamiliki wa mabasi hayo maalum ya kukodi, kuzingatia matumizi sahihi ya kitufe hicho cha utambuzi wa dereva na kwamba madereva wasio kifaa hicho, wanatakiwa kufika katika ofisi za LATRA katika maeneo yao ili wasajiliwe na kuunganishwa katika mfumo.

Pazzy alisema ili kurahisisha kazi hiyo, mamlaka itafanya usajili wa vitufe vya utambuzi wa dereva kwenye baadhi ya maeneo ya barabara ambayo mabasi husimama.

Kwa mujibu wa LATRA, mabasi yanayofungwa VTS lengo kubwa ni kuhakikisha magari hasa yanayosafiri umbali mrefu, yanapokuwa barabarani, kufuatiliwa kwa ukaribu hususani suala la mwendo kasi na mwenendo wa dereva anayeendesha gari.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Patrick Sawala (katikati) akipokea nakala ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2034-2024) kutoka kwa Kaimu Meneja Usaidizi wa Kiufundi kwa Waendelezaji Miradi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Emanuel Yesaya (kushoto). Kulia ni Msimamizi wa Mradi kwa Mkoa huo kutoka REA, Aziz Abbu wakati wa kutambulisha mradi wa kusambaza majiko ya gesi ya kilo sita kwa bei ya ruzuku mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva wataka kuboreshewa miundombinu ya kituo

**Na Benny Kingson,** TABORA

UONGOZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora umetakiwa kuwatendea haki madereva wa magari yanayofanya safari kati ya Tabora mjini na Wilaya za Sikonge Uyui na Urambo kwa kuboresha miundombinu ya kituo cha magari kilichopo eneo la maduka 30 mjini hapa kwa madai ya kuwanyima uhuru, amani na usalama wa kufanya kazi.

Katibu Msaidizi wa Umoja wa madereva mkoani hapa (UWAMATA), Charles Nyabala, aliiambia Nipashe kuwa eneo hilo katika kipindi cha masika linajaa maji ya mvua kutokana na mashimo mengi.

Alisema kuwa walihamishiwa eneo hilo lenye maduka 30 ya manispaa ili kuchangamsha mzunguko wa biashara wakitokea kando ya barabara iendayo wilayani Sikonge na waliahidiwa kuwekewa miundombinu bora na mazingira mazuri, lakini hakuna kilichofanyika na badala yake ni kero kwao.

"Angalia mashimo yaliyopo hapa yamejaa tope na maji katika eneo lote hili, mvua zikinyesha maji yanajaa na kufika magotini, je tunafanyaje kazi, abiria wanakujaje kupanda magari au wanashukaje wakifika, ushuru wanachukua kila siku, lakini hawatujali kabisa," alisema.

Alisema kila siku manispaa wanaongeza kujenga mabanda na kupunguza eneo la kituo kwa kuzingatia kuwa yapo magari kati ya 50 hadi 70 yanayotoa huduma eneo hilo kutokea mjini humo kwenda wilayani Sikonge, Uyui na Urambo na pia kuna shughuli nyingine zinafanywa ambazo ni hatari kwa usalama wa magari na maisha ya watu.

Juma Rajabu na Musa Bundala, madereva wa magari wa eneo hilo walisema kuna mamalishe waliopo kituoni hapo wanaofanya shughuli zao ambazo zinatumia moto zinazoweza kuleta madhara makubwa kama hatua za haraka hazitochuliwa na mamlaka husika.

Walisema kuwa hata askari wa kikosi cha Jeshi la Zimamoto na Ukoaji waliopo eneo hilo hawachukui tahadhari yoyote kuhusu mamalishe hao, kazi yao ni kukagua magari kama ya vifaa vya kuzima moto na kama huna wanawapiga faini, lakini hawaangalii suala la moto unaowashwa na mama lishe kituoni hapo.

Dereva Erick Deogratias na Ednul Salum, walisema wanasikitishwa na uongozi wa manispaa hiyo kuendelea kujenga vibanda kituoni hapo na kupunguza eneo na kwamba wamekuwa wakifanya hivyo kwa kuwakomoa, kwa kuwa wamekuwa wakijenga nyakati za usiku kwa kuvizia na kusimamiwa na askari wa Jeshi la akiba (mgambo) pamoja na viongozi wao.

Uchunguzi umebaini kuna baadhi ya maofisa wa Manispaa hiyo wamekuwa wakifanya kazi kwa matakwa ya watu na maslahi yao na kwamba kunahitajika kuchukuliwa hatua za haraka kurekebisha kasoro zote, kuweka sawa suala la usalama na kufuatilia ujenzi wa kinyemela wa vibanda unaoendelea kupunguza eneo la kituo hicho.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Elias Kayandabila, alipotafutwa kutoa ufafanuzi wa changamoto hizo alisema yupo likizo lakini aliahidi kuwaagiza wasaidizi wake kushughulikia atakaporejea kazini, kusimamia na kuchukua hatua haraka kupata ufumbuzi wa kudumu.

# Watanzania watakiwa kulinda amani, utulivu

**Na Steven William,** MUHEZA

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Tanga, Elias Majo, amewahimiza Watanzania kuheshimu, kulinda amani na utulivu nchini.

Wito huo aliutoa juzi katika Ibada kanisani hapo.

Alisisitiza kusameheana kutokana na upungufu wa kibinadamu na kuanza mwaka mpya wa 2025 kwa upendo, mshikamano na amani pamoja na kuiombea nchi amani na Rais Samia Suluhu.

Alisema anamshukuru Mungu kwa kujalia kuwafikisha mwaka mpya na kujitathmini kuanzia kaya, wilaya, mkoa hadi taifa kuendelea kumshukuru Mungu kwa kuwafikisha.

Askofu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Dk. Msafiri Mbilu, aliwahimiza wakristo kuendelea kumuomba Mungu aweke baraka zake kwa Watanzania ili mwaka 2025 uwe wenye baraka.

Aliyasema hayo katika taarifa ya Askofu iliyosomwa na Katibu Mkuu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Julius Madiga Katika ibada kuu ya kuukaribisha mwaka mpya.

Padri wa Kanisa Katoliki la Kristo Mfufuka wilayani Muheza, Martine Kihiyo aliendelea kuwahimiza watanzania kuheshimu, kulinda amani na utulivu katika nchi badala ya kutumika kuharibu tunu hiyo muhimu akisistiza kusameheana na kuanza mwaka upya kwa upendo na mshikamano.

"Sisi hatuna cha kumlipa Mungu zaidi ya kufanya toba, majuto na kujiongeza zaidi kumjua Mungu na uwe mwaka wa kudumisha amani sio kupanga kuvuruga kama tumeishi vyema mwaka uliopita tujiulize tulitumia vigezo gani kuwa salama hadi sasa? Alisema.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba, Paul Luhinga alisema ipo sababu ya kila mmoja kumshukuru Mungu kwa kuingia mwaka 2025 kusherehekea kwa amani.

"Nitoe salamu za heri ya mwaka mpya na tunapoanza mwaka mpya waumini wa imani zote tufanye kazi kwa bidii kuunga juhudi za serikali ya kuinua uchumi wetu, wazazi na walezi nao niwasihi kuwalea watoto wao katika maadili mema kwa kuwa ndiyo nguvu kazi ya taifa kwa siku zijazo," alifafanua mchungaji Luhinga.

# HADITHI

# Malaika shetani-2

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo hukupata kudhani. Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana. Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini. Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa. Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wanakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**




Kitu ambacho ndugu wengi walichoshukuru ni kupatikana kwa mwili wa Naima, angalau uzikwe na heshima kama binadamu tofauti na kama ungefukiwa na wauaji.

Muda wa kwenda mazikoni ukawadia na watu wengi walishiriki mazishi ya binti huyo, kila mmoja akimtukuza mwenyezi Mungu.

"Hata binti mzuri na mrembo kama huyo anakufa, kweli kifo ni fumbo, kifo ni kwa kila mtu, haijalishi mzuri na mbaya, masikini na tajiri," alisikika mama mmoja mtu mzima.

"Naima mwenye uzuri wa kuvutia, sura ya kupendeza, mwili laini, ngozi kama sufi, leo hii mwili wako unalala kwenye udongo?" Alisikika akisema kijana mmoja ambaye haikujulikana alikuwa anauliza au anaomboleza baada ya kuona mwili wa Naima unashushwa kaburini.

Baada ya maneno hayo alionekana kushindwa kujizuia, akaangua kilio. Rafiki zake akamshika na kumpeleka pembeni kidogo huku wakimbembeleza.

Kijana huyo alikuwa mmoja wa vijana wengi waliojaribu kumtaka Naima kimapenzi. Lakini aligonga mwamba. Pamoja na kugonga mwamba aliendelea kuheshimu hisia za msichana huyo, pia aliendelea kumpenda na kila anapomuona moyo wake kulipuka. Naima alikuwa akiwaambia wote wanaomtaka kuwa yeye ni bado mwanafunzi, bado mdogo na hawezi kujiingia kwenye masuala ya mahusiano kwani ana ndoto zake kwenye maisha yake ya baadaye. Yoyote anayemtaka kweli amsubiri mpaka pale atakapotimiza ndoto zake atakapomaliza kusomea udaktari.

Hii ilisababisha vijana wengine na hata baadhi ya watu wazima kumchukia, lakini wapo waliokubaliana na anachokitaka mwenyewe na waliendelea kushirikiana naye.

Kwa bahati mzuri alikuwa ni msichana mcheshi mwenye heshima kwa kila mtu. Hicho kilisababisha hata wale waliomchukia kwa sababu tu ya kukataliwa kuendelea kumpenda. Labda kwa kudhani ipo siku atabadili mawazo yake.

Mwili wa Naima ulizikwa jioni siku hiyo ukihudhuriwa na umati mkubwa wa watu ambao walionekana kuwa na huzuni iliyojionyesha wazi.

Wakubwa na watoto walionekana kuwa na huzuni, wengine wakibubujikwa na machozi dhahiri na wengine kimya kimya.

**Kikubwa hapo ni kwamba hata aliyewatuma vijana wataokwenda kutekeleza mauaji ya Naima naye hajui kisa chochote. Amebebwa na tamaa ya pesa tu.**

Wengine hasa vijana walionekana kuwa na hasira, wakidai waliofanya hivyo watafutwe haraka sana, kama ni kutoka kijiji kile au kingine msako lazima ufanywe.

Hilo lilijidhihirisha wazi kiasi kwamba wakaapa hata kama sungusungu au mgambo wa kijiji hawawezi kufanya hivyo, vijana wenyewe walisema wako tayari kuifanya tena bila malipo yoyote.

Hali hiyo iliwafanya viongozi kutoa hotuba ya kuwapoza watu kwenye mazishi ili kazi hiyo ifanywe na watu wenye mamlaka na si vinginevyo.

"Ndugu wanakijiji, najua wote mnavyojisikia baada ya kutokea msiba huu mzito. Mimi kama Mwenyekiti wa Kijiji hiki cha Mikamba, nawaomba tusiwe na mihemko. Siku zote ukiwa na hasira au mhemko huwezi kulifanya jambo kwa usahihi. Jambo limeshatokea. Hatujui ni kitu gani kimempata mwenzetu. Kwa hiyo tuviachie vyombo vya sheria. Hapa kuna mgambo wa kijiji, kuna sungusungu. Baada ya msiba huu tutakaa na ndugu ili tuone tuanzie wapi kuhusu suala hili. Kusema kweli limetuuma, limutuhuzunisha na limetusikitisha kama wanakijiji. Tunawaomba hata wenzetu wa vijiji vya jirani. Wakiona chochote kile ambacho kinaweza kuwa na ushahidi wa hili lililotokea watueleze. Kwa sasa tuwe watulivu. Tukitoka hapa twende majumbani kwetu na kuviachie vyombo vyetu," alisema mwenyekiti hiyo Bozi Tamim.

Hotuba hiyo kwa kiasi kikubwa ilionekana kuwatuliza vijana wenye hasira ambao walidhimia kuanza msako siku hiyo hiyo. Hata hivyo ukiwauliza wenyewe wangeanzia wapi wangeshindwa kukuambia.

==========================

"Nadhani mmeelewa." "Tumeelewa." "Msichana huwa ana kawaida ya kwenda kwa mjomba wake kila Jumamosi asubuhi. Tumeangalia siku zingine ni kwamba akienda shuleni huwa anaongozana na wenzake. Akirudi na wenzake pia. Kisimani anakwenda na wadogo zake, na hata akiwa peke yake, njia ya kisimani siku zote siyo salama kwa sababu ina watu wengi wanaopita hivyo ni hatari sana."Msemaji alisikika akiwaambia anaowatuma.

"Sawa, sasa unataka tumuue wakati gani, anaokwenda au kurudi?" Alisikika mwingine.

"Wakati wa kurudi. Asubuhi si nyakati nzuri sana, wakati mwingine kunakuwa na watu, lakini jioni anaporejea hasa Jumamosi kunakuwa hakuna watu wengi na hasa kwenye kile kipori ambacho kinatenganisha kijiji cha Mikwambe na Matuo. Mjomba wake akiishi Matuo."

Kilikuwa ni kikao cha watu wanne, ambacho ndicho kilichoandaa mpango wa kutoa uhai wa Naima.

"Sababu hasa ya kumuua huyo binti ni nini?" Mmoja akauliza. Yule aliyeonekana ndiyo anawatuma akamtazama kwa macho makali.

"Wewe siyo mtaalamu wa mambo haya eee. Umeanza lini hii kazi? Halo! Akawageukia wenzake wawili, huyu ameanza lini hii kazi? Huwa hatuulizi kwa nini. Umepewa tenda ya kuua mtu au kumdhuru, unachotakiwa kufanya wewe ni kuhakikisha malipo yako yanakamilika kwa jinsi mlivyoahidiana, siyo kuuliza sababu. Haya kama ukiambiwa sababu ndiyo unakwenda kumponya, au kumuua mara mbili?" Hakuna aliyejibu. Walibaki wanamtazama.

"Ni hivi, kila mmoja amepata chake. Kila mmoja amepata nusu ya malipo. Kila mmoja ana shilingi laki tatu hapo nimeshawapa, na kazi ikimalizika mnamaliziwa laki mbili kila mmoja. Hilo ndilo la muhimu. Sabubu huwezi kuijua. Mimi mwenyewe hapa siijui sababu ya kuuawa huyu denti Naima. Kuna bosi amenipa hii tenda na wala sijamuuliza kwa nini. Ameniambia nitafute vijana wa kazi, nimewapata nyinyi, najua mtaifanya. Kisa nini? Atajua mwenyewe, hapa kila mmoja amepata chake, maisha yanaendelea. Kama siku nyingine atakuwa na mtu mwingine anataka kumfuta kwenye uso wa dunia, ataniita na mimi nitawafuata," alisema na kueleweka.

Kikubwa hapo ni kwamba hata aliyewatuma vijana wataokwenda kutekeleza mauaji ya Naima naye hajui kisa chochote. Amebebwa na tamaa ya pesa tu.

Walikutana chini ya mti mmoja mkubwa, maeneo ya kando ya kijiji cha Mikwambe na Matuo. Walikana hapo ili mipango yao isivuje na kujulikana. Na wakaahidiana baada ya tukio watakutana tena hapo kwa ajili ya kumaliziana malipo yaliyobaki.

Wauaji hao wote walikuwa wametoka kwenye vijiji tofauti vya mbali. Baada ya kupatikana mmoja, alianza kuwakusanya wenzake anaowafahamu, ambao huwa wanatumiwa na watu mbalimbali wabaya kuwadhuru, kuwaumiza au kuua watu kwenye vijiji mbalimbali huko Bingu.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# MGUNDA AENDELEA KUPITISHA FAGIO LA WACHEZAJI NAMUNGO

Na Adam Fungamwango

KIUNGO mkongwe nchini, Frank Domayo, ni mmoja kati ya wachezaji wanne waliotemwa na uongozi wa Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kupisha usajili wa wachezaji wapya ndani ya timu hiyo, imethibitishwa.

Taarifa rasmi ya klabu hiyo iliyotolewa jana imesema mbali na Domayo, ambaye aliwahi kuzichezea Yanga na Azam FC, wachezaji wengine walioachwa ni Amza Moubarack, Ritch Nkoli na Djuma Shaaban.

Wiki moja iliyopita, Djuma, beki wa kulia wa zamani wa Yanga na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), alisema alimomba kuachwa mwenyewe ili akauguze majeraha yake kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza ndani ya kikosi hicho, lakini klabu ilikuwa haijatoa taarifa rasmi.

"Ahsante Domayo, kiungo chumvi kwa utumishi wako ndani ya familia ya wauaji wa kusini kwa kipindi cha misimu miwili. Tunakutakiwa kila la heri katika majukumu yako mapya," ilisema taarifa ya klabu hiyo yenye makao yake Ruangwa mkoani, Lindi.

Domayo alijiunga na Namungo Januari Mosi, mwaka 2023, akitokea Azam ambapo kabla ya hapo alikuwa akikitumikia kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

Mabingwa hao watetezi, walimsajili Domayo Julai Mosi mwaka, 2012 kutoka klabu ya JKT Ruvu (sasa JKT Tanzania), ambapo aliitumikia hadi Julai Mosi mwaka, 2014, alipotimkia Azam.

Wachezaji walioachwa na Namungo wanapishana na wachezaji ambao wamesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Wachezaji hao ni pamoja na Derrick Mukombozi na Emmanuel Charles ambayo waliichezea timu hiyo msimu uliopita walikuwa katika kikosi hicho lakini kwa namna ambayo haijafahamika, hawakusajiliwa mwanzoni mwa msimu huu.

Mchezaji mwingine aliyeingia kipindi hiki cha usajili ni Najim Mussa ambaye yupo kwa mkopo akitokea Singida Black Stars ya mkoani, Singida.

Namungo haijafanya vizuri sana katika michezo yake ya mzunguko wa kwanza, ikiwa tayari imeshacheza michezo 16, ikiwa nafasi ya 12 baada ya kujikusanyia pointi 17 kibindoni.

Timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), zinaendelea kujiimarisha katika dirisha dogo la usajili ili kufikia malengo ya kumaliza vyema msimu wa mwaka 2024/2025.

Mzunguko wa pili wa Ligi Kuu utanarajiwa kuanza ifikapo Machi Mosi, mwaka huu baada ya kupisha fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kumalizika.



Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Simba Queens, Mkenya Elizabeth Wambui (kushoto), akimtoka mchezaji wa Allinace Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza hivi karibuni. Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 5-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Warriors, Afya uso kwa uso

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya netiboli ya Warriors inatarajia kukutana na Afya katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Gykhana Visiwani hapa.

Timu tisa kutoka Unguja zinatarajiwa kushiriki mashindano hayo ambazo ni Warriors, Afya, KVZ, Mafunzo, NHIF, Zimamoto, Bandari, Shaurimoyo na JKU.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Zanzibar (CHANEZA), Said Mansab, alisema wanaendelea vyema na maandalizi kuhusiana na michunao hayo ambayo wanatarajia yatakuwa na ushindani.

Mansab alisema tayari wamepeleka barua kwa wadau mbalimbali wa michezo ili kuomba misaada ya kufanikisha michuano hiyo inachezwa kwa ufanisi.

"Michuano ya mwaka huu tumepanga kuchezwa kwa aina yake kutokana na hamasa kubwa iliyoonekana katika Ligi ya Netball visiwani hapa, kila mwaka tumekuwa tukifanya maboresho katika mashindano haya kwa kuangalia changamoto za miaka iliyopita, hivyo msimu huu tumejipanga kuwa na mashindano mazuri na yenye ushindani," alisema Mansab.

Alimtaja mgeni rasmi katika ufunguzi wa michuano hiyo anatarajiwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Jinsia, Wanawake na Watoto, Anna Athanas Paul.

## Stand United yanasa nyota wapya wanne

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Stand United imesajili wachezaji wapya wanne kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao kinachoshiriki Ligi ya Championship.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema wachezaji iliyowaongeza kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili ni pamoja na Omari Issa, Anicet Revocatus, Ramadhani Said na Ashraf Malolo.

"Tumewasajili wachezaji hawa kwa sababau tunaamini watakisaidia kikosi chetu katika kampeni ya kutaka kucheza Ligi Kuu msimu ujao, Omari na Anicet ni mastraika ambao tunauhakika watatufungia mabao ya kutosha, Ramadhani ni kiungo na Ashraf ni mchezaji wa timu ya taifa ya vijana chini ya miaka 23 ambaye naye amejiunga nasi kukiongezea nguvu kikosi chetu," ilisema taarifa hiyo.

Tangu Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), ilipofungua dirisha dogo la usajili hapo Desemba 15, mwaka jana, timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, wanaume na wanawake, Ligi ya Championship na First League, zimekuwa katika heka heka za kusajili wachezaji kwa ajili ya kuongeza kwenye vikosi vyao.

Stand United ambayo ilishuka daraja msimu wa 2020/2021, inashika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi ya Championship ambapo imeingia kwenye raundi ya 14.

Timu hiyo ina pointi 30 baada ya kucheza michezo 14, imeshinda mechi tisa, sare tatu na kupoteza miwili.

**Katika ligi hiyo, timu mbili zitakazomaliza na fasi ya juu zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2025/2026, huku ya tatu na ya nne zikicheza mechi za mchujo, mshindi akisubiri timu itakayoshinda 'play off' dhidi ya klabu ya Ligi Kuu.**

Mtibwa Sugar yenye pointi 35 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Mbeya City yenye pointi 31 huku Geita Gold yenye pointi 30 iko kwenye nafasi ya tatu huku Biashara United yenye pointi moja inaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OLMO AGOMBEWA EPL
JARIBIO la Barcelona lililoshindwa la kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo, kwa kipindi cha pili cha msimu limefungua milango kwa Manchester United na Manchester City kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 bila malipo.***(Mundo Deportivo)***

### TRENT ANUKIA MADRID
REAL Madrid ingependelea kumsajili beki wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold (26), katika dirisha la Januari, lakini wako tayari kusubiri hadi msimu wa majira ya joto wakati mkataba wake utakapomalizika ikiwa Liverpool hawataki kumuuza mchezaji huyo mwezi huu.(***Marca)***

### ISAKA KUBAKI NEWCASTLE
MSHAMBULIAJI wa Newcastle United raia wa Sweden, Alexander Isak yuko tayari kubakia katika klabu hiyo iwapo watamaliza katika nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu msimu huu, na kutoa pigo kwa Arsenal ambao wana nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

### CHELSEA YAMFUTA DELAP
CHELSEA inamfuatilia mshambuliaji wa Ipswich, Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, na mshambuliaji wa Brighton wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye miaka 20, wakati wanatazamia kutoa ushindani kwa mshambuliaji ambaye ni chaguo la kwanza, Nicolas Jackson. ***(Talksport)***

### LOPETEGUI MUDA ZAIDI
KOCHA wa West Ham, Julen Lopetegui atapewa muda zaidi licha ya kiwango kibovu cha wagonga nyundo hao msimu huu. ***(Telegraph)***

### RONALDO HANA UHAKIKA
CRISTIANO Ronaldo amekataa kudhibitisha kama hataondoka Al-Nassr msimu wa kiangazi, huku mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 39 akiwa huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine kuanzia Januari 1. (***Marca)***

### TRAFFORD ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United inapanga kumnunua kipa wa Burnley mwenye umri wa miaka 22, James Trafford kwa kitita cha pauni milioni 20. (***Sun)***

### WOLVES YAMTAKA DONSO
KLABU ya Wolves inataka kumsajili mlinzi wa Lens na Austria, Kevin Danso mwenye umri wa miaka 26 Januari. (***Sky Sports)***

### MCATEE AWEKWA SOKONI
BAYERN Leverkusen ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtazama kwa karibu kiungo wa kati wa Manchester City, mwenye umri wa miaka 22, James McAtee. (***Mail)***

### WERNER KURUDI LEIPZIG
KLABU ya Tottenham Hotspur haina uwezekano wa kubadilisha mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28 kuwa mkataba wa kudumu, na hiyo inamaanisha kwamba atarejea RB Leipzig msimu wa kiangazi. ***(Bild)***

### SAINZ ATAKIWA ATHLETIC
KLABU ya Athletic Bilbao imemtambua kiungo wa kati wa Norwich, Borja Sainz mwenye umri wa miaka 23, kama kiungo mbadala bora wa Nico Williams, iwapo winga huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 22 ataondoka katika klabu hiyo msimu wa kiangazi. (***Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RODRI ATEMA CHECHE KUHUSU BALLON D'OR

**MADRID,** Hispania

**●●● Mshindi huyo asema anashangazwa Ronaldo hakubaliani na ushindi...**

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Rodri amesema haelewi kwa nini mshambuliaji nyota, Cristiano Ronaldo, ametilia shaka uteuzi wake kama mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or 2024.

**Mshindi mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, Ronaldo alisema Vinícius Júnior alistahili tuzo hiyo dhidi ya Rodri kwa sababu fowadi huyo wa Real Madrid alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufunga katika mechi ya fainali.**

Alipoulizwa kuhusu maoni ya Ronaldo, Rodri aliiambia Diario AS: "Nashangaa, kwa kweli, kwa sababu anajua jinsi tuzo hii inavyofanya kazi na zaidi ya yote, jinsi mshindi anavyochaguliwa.

"Waandishi wa habari waliopiga kura wameona mimi nishinde. Pengine waandishi hao hao ndio wakati fulani walimpigia kura ili yeye ashinde, na nadhani basi atakubali."

Real Madrid walisusia sherehe za Ballon d'Or jijini, Paris Oktoba, mwaka jana baada ya Rodri kupokea tuzo hiyo.

Rodri mwenye umri wa miaka 28, alitunukiwa tuzo hiyo ya kifahari baada ya msimu mzuri ambao ulimfanya kushinda taji la Ligi Kuu England akiwa na City na ubingwa wa michuano ya Ulaya akiwa na Hispania.

Vinícius alikuwa mshindani mkuu wa kushinda tuzo hiyo baada ya kuisaidia Madrid kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil baadaye alitunukiwa tuzo ya mchezaji bora wa kiume wa FIFA na kushinda tuzo ya Globe Soccer ya wanaume Desemba 30, mwaka jana.

Rodri, ambaye aliumia misuli ya paja Septemba, mwaka jana alizungumzia mchango wa kushinda Ballon d'Or imekuwa nayo katika maisha yake ya kila siku.

"Imebadilisha maisha yangu," alisema. "Mambo mengi ambayo ningeweza kufanya hapo awali, ni wazi, siwezi tena kufanya. Lakini jamani, ni kwa sababu nzuri ... nina falsafa katika maisha lazima uchukue vitu kama unavyopewa."

# DE JONG AANIKA SIRI KUHUSU MATAJI BARCA




**BARCELONA,** Hispania

FRENKIE de Jong amesema - amesikitishwa na jinsi mataji machache aliyoshinda akiwa na Barcelona na atabakia katika klabu hiyo ikiwa anahisi bado anaweza kuchangia kitu uwanjani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alijiunga na Barca akitokea Ajax mwaka 2019 lakini ameshinda mataji matatu pekee, LaLiga moja, Copa del Rey na Supercopa na amekuwa akisumbuliwa na matatizo ya kifundo cha mguu katika misimu miwili iliyopita.

"Barca ilikuwa na ndiyo klabu ya ndoto yangu," alisema De Jong katika mahojiano na Voetbal International.

"Kama kijana mdogo, nilitaka kucheza hapa. Bado ninafurahia kila siku katika klabu hii, lakini kama ilivyo katika maisha halisi, sio kila kitu ni bora kama unavyofikiria.

"Kuna sababu wanasema usiwahi kukutana na mashujaa wako, sivyo? Lazima nikiri wakati nasaini mkataba wangu hapa, sikufikiria baada ya miaka mitano ningeshinda LaLiga moja tu, Copa del Rey na Supercopa moja.

"Nilifikiri angalau mara mbili, hivyo inakatisha tamaa. Lakini kila mara mambo hutokea ambayo huwezi kutabiri kabla."

De Jong kwa sasa anapitia kipindi kigumu zaidi cha wakati wake katika klabu hiyo ya Catalan baada ya kusumbuliwa na majeraha ya kifundo cha mguu msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amezungumza kuhusu majeraha hayo yamemsababishia kiwewe.

Hapo awali alikataa ofa za kuondoka katika klabu hiyo, ikiwa ni pamoja na kutoka kwa Manchester United mnamo mwaka 2022, lakini anasema angefikiria kuondoka ikiwa anahisi sio kiwango kinachohitajika.

"Mara nyingi watu hufikiri nataka kubaki Barcelona milele kwa sababu ninaishi vizuri sana hapa pamoja na soka," aliongeza.

"Hiyo ni kweli, lakini ni ya pili kwa kile kinachotokea uwanjani.

"Nikigundua siwezi kuonyesha vya kutosha hapa, sichangii au siwezi kushinda chochote na timu, nisingekuwa hapa tena.

"Niko njia panda katika maisha yangu ya soka. Bado nina mwaka mmoja na nusu Barcelona na unasoma kwenye magazeti kuwa hili ni suala, kwangu si sawa kwa sasa."

## Rashford Marcus avunja ukimya

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford amejibu kuhusu uvumi wa yeye kuondoka Manchester United akisema huo ni upuuzi.


Akiwa ameondolewa katika vikosi vinne vya Ruben Amorim siku ya mechi Desemba - kipindi ambacho pia alikiri nia yake ya kuhitaji changamoto mpya - Rashford anaaminika atabaki.

Ripoti nchini England zilidai Rashford aliomba usaidizi wa wakala mpya kujaribu kulazimisha kuondoka United, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ametupilia mbali uvumi huo katika mitandao ya kijamii.

"Kumekuwa na habari nyingi za uongo zilizoandikwa katika wiki chache zilizopita, lakini jamani, hii inazidi kuwa kejeli," alisema.

"Sijawahi kukutana na yoyote na sina mpango wowote wa kufanya hivyo."

Hata hivyo, Rashford bado anapatikana ikiwa mshambuliaji yoyote anataka kujitokeza na kufikia bei inayotakiwa na United, ambayo inaaminika karibu pauni milioni 40.




## Ancelotti hajaamua kusajili Januari



**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema "tutaona" ikiwa Real Madrid wanaweza kufanya usajili Januari hii, baada ya wababe hao wa LaLiga kuonyesha nia ya kumchukua Trent Alexander-Arnold.

ESPN iliripoti Jumanne vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool walikataa haraka uhamisho wa Januari wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England, ambaye ni shabaha kuu ya Madrid msimu ujao wa joto wakati mkataba wake unapomalizika kule Anfield.

Ancelotti amesita kuzungumzia iwapo angependa kuona nyongeza kwenye kikosi chake mwezi huu, huku beki chaguo la kwanza wa kulia Dani Carvajal akiondolewa kwa msimu huu kutokana na jeraha baya la goti.

"Kuzungumza juu ya hilo ni ngumu," alisema Ancelotti.

"Tutaona. Hilo ndilo jambo pekee ninaloweza kusema. Tuna michezo mingi Januari, tumezingatia hilo. Kuzungumza kuhusu soko sio moja kwa moja kwangu hivi sasa."

Madrid walikuwa wakihusishwa na Alexander-Arnold hata kabla ya Carvajal kuumia kwa muda mrefu, lakini kukosekana kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kumeongeza hali ya dharura katika suala hilo.

"Sitaki kulizungumzia kwa sababu si wakati wa kulizungumzia hapa," alisema Ancelotti.

"Nimesema tutaona. Nimefurahishwa na kikosi tulichonacho. Tumekuwa na matatizo, lakini siku zote tumeweza kuyashinda."

Madrid wamekumbwa na mfululizo wa majeraha msimu huu, ingawa wasiwasi huo umepunguzwa na kurejea mazoezini kwa beki wa kati David Alaba.

"Sasa tuna mechi za kushinda," aliongeza Ancelotti.

"Timu imeitikia vizuri na sasa ina ari zaidi, imesisimka, na iko katika hali nzuri zaidi. Wachezaji wamerudi, Alaba ameanza mazoezi na sisi. Hivyo kwa sasa hali ni nzuri na tunapaswa kudumisha hali hiyo nzuri, na sisi. inaweza tu kufanya hivyo kwa kushinda mechi."

HABARI MICHEZO

## Yanga kazi moja...

INATOKA UKURASA 24

Al Hilal na ilipoenda ugenini Algeria ilifungwa tena idadi kama hiyo ya mabao.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ni Simba ambayo kesho itashuka ugenini Tunisia kucheza dhidi ya CS Sfaxien ya huko.

## Simba yaitaka robo fainali CAF mapema

INATOKA UKURASA 24

nchi mbalimbali, wiki kadhaa tulitoka kucheza Algeria na Constantine, kulikuwa na hali ya hewa ya baridi kama hii, tena afadhali ya hii, ya huku kidogo imepoa tofauti na kule," Zimbwe Jr alisema.

Naye kiungo mkongwe, Mzamiru Yassin, alisema kwa misimu kadhaa wamekuwa wakisubiria hadi mchezo wa mwisho ili kuamua hatima ya kucheza hatua ya robo fainali, lakini safari hii wanahitaji kuona wanakamilisha kibarua hicho mapema.

Mzamiru alisema ingawa wanajua mechi itakuwa ngumu lakini yeye hana wasiwasi wa hali ya hewa, wala ugeni kwa sababu wameshacheza kwenye uwanja huo mara kadhaa akiwa na kikosi cha timu ya taifa, (Taifa Stars).

"Kwangu mimi ni mzoefu, haitakuwa mara ya kwanza kucheza kwenye uwanja huu, hivyo ni mwenyeji, nimewahi kuwa hapa mara kadhaa nikiwa na kikosi cha timu ya taifa, hata hali ya hewa ya baridi hainisumbui, pamoja na hayo siku zote mechi ya ugenini zinakuwa ngumu, haijalishi mnacheza na nani, muhimu ni kuwa makini, yoyote atakayepata dakika za kucheza azitumikie ipasavyo," alisema Mzamiru.

Wakati wachezaji wakisema hayo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema wamefanya mazoezi mara tatu wakiwa huko na wanachomalizia ni mpango mkakati jinsi ya kuicheza mechi hiyo.

"Tunajaribu kuzoea hali ya hewa ya hapa, lakini kikubwa ni kutengeneza mpango mkakati wa mchezo wenyewe na jinsi ya kwenda kukabiliana na CS Sfaxien, kwa vile tulivyowaona na kuwasoma wanavyocheza," alisema Fadlu.

Simba inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi sita sawa na CS Constantine na Bravo do Maquis ya Angola, huku CS Sfaxien ikiwa haina pointi yoyote mpaka sasa katika kundi lao.

# MBABE WA YANGA AKARIBIA KUTUA KMC FC DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imetajwa iko katika mazungumzo ya kupata saini ya winga wa Azam FC, Cheickna Diakite, na Offen Chikola wa Tabora United kwa ajili ya kukiboresha kikosi chao kipindi hiki cha dirisha dogo.

Katika ushindi wa mabao 3-1 ambao Tabora United waliupata dhidi ya Yanga, Chikola alifunga magoli mawili.

Taarifa kutoka KMC FC zinasema klabu hiyo inawania saini za wachezaji hao ikiwa ni mapendekezo ya Kocha Mkuu, Kally Ongalla, ambaye anataka kukiongezea nguvu kikosi kwa kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa kutokana na ugumu wa ligi.

Chanzo kimesema KMC ina nafasi kubwa ya kumchukua Diakite, raia wa Mali, baada ya yeye mwenyewe kuomba atolewe hata kwa mkopo kwenda katika timu ambayo itampa nafasi zaidi ya kucheza kwa sababu kwa sasa amekuwa akisugua benchi kwenye kikosi cha Azam.

"Nadhani kwa Diakite ni rahisi zaidi kumpata kwa mkopo wa miezi sita, kwa sababu yeye mwenyewe amekuwa akishinikiza uongozi umtoe kwa mkopo kwa sababu amekuwa hapati nafasi ya kucheza, kwa upande wa Chikola, mazungumzo bado yanaendelea kwa sababu ni mmoja wa wachezaji tegemeo wa Tabora, hawawezi kumuachia kwa urahisi," kilisema chanzo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa KMC, Daniel Mwakasungula, amesema kwa sasa hawezi kuwataja wachezaji wanaowahitaji kipindi cha dirisha dogo la usajili ingawa taratibu za kusajili baadhi ya wachezaji kutokana na mapendekezo ya benchi la ufundi zimeshaanza.

"Tunataka kuboresha maeneo machache tu, hatutaacha wachezaji wengi, watakaoingia ni vijana ambao tunaamini wana kiu na uchu wa kufikia mafanikio, tukikamilisha tutaweka wazi," alisema Mwakasungula.

Mpaka Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama, ikiwa imemaliza mzunguko wa kwanza, KMC ipo nafasi ya 10, ikiwa imekusanya pointi 19, ikicheza michezo 16, ikipata ushindi mechi tano, sare nne na kupoteza michezo saba.



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Leonel Ateba, Che Malone Fondoh (katikati) na Mohammed Hussein (Zimbwe Jr), wakifurahi baada ya kumaliza mazoezi kwa ajili ya mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji, CS Sfaxien itakayochezwa kesho nchini Tunisia. **PICHA: SIMBA SC**

# Raizin atajwa Kagera Sugar

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa Mtibwa Sugar, ambaye anawaniwa kwa udi na uvumba na Kagera Sugar inayoshiriki Ligi Kuu, Raizin Hafidh, ameendelea kuwa tishio katika Ligi ya Championship baada ya kufikisha mabao 11 hadi kufikia raundi ya 14.

Mabao aliyofunga mchezaji huyo kwa kiasi kikubwa yameifanya Mtibwa Sugar kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo, ikifikisha pointi 35.

Kwa mujibu wa takwimu iliyotolewa juzi na Bodi ya Ligi, Raizin anafuatiwa na Abdulaziz Shahame wa TMA aliyefunga mabao tisa huku straika wa zamani wa Azam, Ihefu FC na Coastal Union, Andrew Simchimba, ambaye kwa sasa anaichezea Geita Gold amefunga mabao nane huku Msenda Amri wa Stand United, Naku James wa Mbuni FC na Seif Adam wa Mbeya Kwanza, wote wakipachika mabao sita kila mmoja.

Habari zinasema Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Melis Medo, ambaye aliifundisha Mtibwa Sugar katika mechi kadhaa ya Ligi ya Championship, amewaambia mabosi wa timu yake anamhitaji Raizin kwa ajili ya kuboresha kikosi chake.

Raizin, kabla ya kuichezea Mtibwa Sugar, amewahi kuichezea Gwambia FC, African Lyon, Coastal Union na Dodoma Jiji wakati zipo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo huo, vita kali katika ligi hiyo ni ya kuwania nafasi ya pili ambapo Mbeya City imewaengua Geita Gold iliyokuwa ikiishikilia kwa muda mrefu.

Michezo

Nipashe

Jumamosi Januari 4, 2025



Rashford Marcus avunja ukimya UKURASA 22

# Yanga SC kazi moja ushindi

●●● Ramovic atamba wamejipanga imara kuwabana Mazembe dakika zote...



Max Nzengeli

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

MASHAMBULIZI mwanzo mwisho, hayo ni maneno ya wawakilishi wa Tanzania, Yanga kuelekea mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe kutoka DR Congo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo Yanga itashuka ikiwa na kazi moja tu ya kuhakikisha inapata ushindi ili kuweka hai matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo.

Timu hizo zilipokutana katika mchezo wa raundi ya tatu uliopigwa kwenye Uwanja wa Mazembe, Mjini Lubumbashi Desemba 14, mwaka jana, zilitoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ameahidi kutowapa 'pumzi' wapinzani wao kwa kufanya mashambulizi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mchezo huo ili kutimiza malengo.

Ramovic alisema hawajui wapinzani wao watacheza vipi, lakini wamejiandaa kuwadhibiti, kuwabana na kutowapa nafasi ya 'kupumua' kwa kutengeneza nafasi za kufunga muda wote wa mchezo huo.

"Nilipokuja wiki sita zilizopita niliona timu imekosa utimamu wa mwili, lakini ni kama wiki nne sasa, nimeongeza nidhamu ya mazoezi na sasa unaona taratibu timu inarejea. Katika mchezo huu pengine TP Mazembe watacheza aina ile ile ya mipira mirefu na krosi katika boksi, lakini tumejiandaa vizuri na wachezaji wameanza kushikamana kama timu, na hii inanipa sana faraja kama kocha.

Tunahitaji kucheza kwa kasi ya hatari, tunahitaji kutompa mwanya mpinzani wetu wala kupumua, kuna namna tumesogea ila bado hatujafika ninapotaka, mashabiki wajue tunataka kushambulia mpaka mwisho, hatutaki kumpa muda wala nafasi mpinzani wetu kufikiria chochote," Ramovic alisema.

Naye Kocha Mkuu wa TP Mazembe, Lamine Ndiaye, aliliambia gazeti hili matokeo ya sare ya bao 1-1 katika mechi iliyopita hayakupokewa vizuri na viongozi na mashabiki wa timu hiyo, hivyo wamejizatiti kushinda katika mchezo wa leo.

Ndiaye alisema amefanyia kazi mapungufu aliyoyabaini na amejiandaa kupata matokeo mazuri ya ugenini.

"Natumai kesho (leo), tutacheza vizuri na tutapata matokeo," alisema kocha huyo.

Mchezaji wa timu hiyo, Atibu Radjabu, aliwataka mashabiki wa soka nchini wajitokeze kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia kandanda safi litakaloonyeshwa.

"Sisi kwetu mpira ni sherehe, wapinzani wetu nadhani wapo tayari kwa mechi na sisi tupo tayari kwa mchezo huu," alisema mchezaji huyo.

Mara ya mwisho timu hizo kukutana kwenye uwanja huo ilikuwa Februari 19, mwaka 2023 katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi, Yanga ikishinda mabao 3-1, shukrani kwa Kennedy Musonda, Mudathir Yahya na Tuisila Kisinda huku lile la kufutia machozi la TP Mazembe likipachikwa wavuni na Alex Ngonga.

Yanga inashika 'mkia' katika Kundi A ikiwa na pointi moja, huku TP Mazembe yenye pointi mbili ikiwa nafasi ya tatu nyuma ya MC Alger ya Algeria na vinara Al Hilal ya Sudan yenye pointi tisa.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walianza hatua ya makundi kwa kukubali kufungwa mabao 2-0, nyumbani na

INAENDELEA UK. 23

# Simba yaitaka robo fainali CAF mapema

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba wamesema watapambana na kujitoa katika kiwango cha juu ili kuhakikisha wanashinda mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien itakayochezwa kesho mapema kwa sababu msimu huu hawataki kusubiri hadi mchezo wa mwisho.

CS Sfaxien itawakaribisha Simba kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi ulioko jijini Tunis kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema katika kikao cha wachezaji wamekubaliana safari hii wanataka kutinga hatua ya robo fainali mapema zaidi na hawataki kusubiri hadi mechi ya mwisho kuamua hatima yao.

"Tumeambizana hatutaki kusubiri hadi mechi za mwisho ndiyo ziamue hatima yetu kila msimu, safari hii tunataka tufuzu mapema, tunakata kushinda hii mechi ili zinazokuja iwe rahisi kwetu, tuwe tunacheza bila presha na mashabiki wetu. Huwa tunaona mechi za mwisho za maamuzi pale Uwanja wa Benjamin Mkapa zinavyokuwa na heka heka," alisema Zimbwe Jr.

Kuhusu hali ya hewa ya baridi, beki huyo alisema haiwezi kuwaathiri kwa sababu wamekuwa ni wazoefu wa kucheza katika nchi mbalimbali kwenye hali kama hiyo.

"Hali ya hewa haiwezi kutuathiri kwa sababu tumeshacheza sana mechi katika hali kama hii

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >